SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
S.L.P 258, Maisara - Zanzibar, Simu: +255 24 2234009, Nukushi: +255 24 2234009
Baruapepe: info@ocagz.go.tz, Tovuti: www.ocagz.go.tz

## DIRA

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi

## DHAMIRA

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa

**Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unapatikana katika matumizi mazuri ya rasilimali za umma Afisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:-**

### Uaminifu

Kuhakikisha Ofisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria.

### Uadilifu

Kuwa ni Ofisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

### Kuwa Huru

Kuwa ni Ofisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria

### Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi

Kuwa ni Ofisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

### Kutunza Siri

Kuwa ni Ofisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

### Uwazi na Uwajibikaji

Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma.

# YALIYOMO

**SURA YA KWANZA**.....................................................................................................1

1.0 UTANGULIZI.....................................................................................................1

1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.....................................................................................................1

1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI.....................................................2

1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI.....................................................3

1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA.................................4

1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI.....................................................4

1.6 SHUKURANI.....................................................................................................5

**SURA YA PILI**.....................................................................................................6

2.0 HATI ZA UKAGUZI.....................................................................................................6

2.1 UTANGULIZI.....................................................................................................6

2.2 AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA.....................................................6

2.3 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....................7

2.4 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....................................................................................................8

**SURA YA TATU**.....................................................................................................9

3.0 UANZISHWAJI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.............................................9

3.1 KUANZISHWA KWA MAMLAKA KWA MUJIBU WA SHERIA.........................................9

3.2 LENGO LA KUANZISHWA KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA..............................9

3.3 UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA...................................9

**SURA YA NNE**.....................................................................................................11

4.0 MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.......11

4.1 BARAZA LA MANISPAA YA MJINI.........................................................................11

4.2 BARAZA LA MANISPAA YA WILAYA YA MAGHARIBI "A"...........................................20

4.3 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"............................................................24

4.4 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "A"........................................................30

4.5 HALMASHAURI YA WILAYA YAKASKAZINI "B"........................................................38

4.6 HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI.....................................................................44

4.7 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI...........................................................50

4.8 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE...........................................................................58

4.9 BARAZA LA MJI MKOANI....................................................................................65

4.10 BARAZA LA MJI WETE......................................................................................70

**SURA YA TANO**....................................................................................................78

5.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA YA HOJA ZA UKAGUZI ZILIZOBAINIKA............................78

5.1 KUIMARISHWA KWA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI...........................................78

5.2 KUFUATWA KWA SHERIA YA MANUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA.........79

5.3 KUWEPO KWA MFUMO WA UDHIBITI WA MALI ZA KUDUMU...................................79

5.4 KUWEPO KWA MFUMO MZURI WA UDHIBITI WA UKUSANYAJI WA MAPATO.............79

5.5 KUWEPO KWA MFUMO WA UTAYARISHAJI WA TAARIFA ZA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA.....................................................................................................79

**VIAMBATISHO**.....................................................................................................81

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu ya 112. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

## 1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu ya 112 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria za fedha, Sheria za manunuzi na sheria nyenginezo.

Kwa mujibu waKifungu ya 112 (3) ya Katiba ya Zanzibar 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

“a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. ”

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za umma.

## 1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleokwa kipindi cha mwaka ulioishia 30 Juni, 2020.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya Ukaguzi na kujiridhisha iwapo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizotayarishwa zitaonyesha sura halisi na sahihi ili kutoa maoni ya ukaguzi juu ya taarifa za mapato na matumizi kama zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Miongoni mwa taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

I. Taarifa ya Mapato na Matumizi
II. Taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu
III. Taarifa ya uwiano na bajeti na kiasi halisi cha matumizi
IV. Sera za uhasibu na maelezo ya taarifa za fedha
V. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Mabaraza ya Manispaa, Miji, na Halmashauri

Kutokana na mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi wa hesabu pamoja na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa kumepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za Umma katika

ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za Umma. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa Sheria mbalimbali zikiwemo sheria za fedha, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, pamoja na Sheria nyenginezo na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

## 1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Katika kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali mbinu na njia mbali mbali za ukaguzi zilitumika ikiwemo taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

1. Kutoa barua za awali za maandalizi ya ukaguzi (Engagement Letter) kwa Taasisi inayokaguliwa.
2. Kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa wa mazingira ya taasisi hiyo ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi.
3. Kuandaa mikakati ya ukaguzi kuanzia mpango wa awali hadi mpango mkuu wa ukaguzi (Pre Planning, Strategic Planing and detailed Planning) itakayozingatia muelekeo na upeo wa ukaguzi ambapo utaonyesha dira na dhamira nzima ya ukaguzi huo.
4. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) pamoja na uongozi wa Taasisi zinazokaguliwa.
5. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbali mbali pamoja na kupata taarifa kutoka kwa wahusika ili kupata uelewa wa kazi za Taasisi zinazokaguliwa.
6. Kutumia njia na mbinu mbali mbali za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Regularity Audit Manual).
7. Kufanya kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit Meeting) na uongozi wa Taasisi inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.
8. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya awali (Management letter) kwa uongozi wa taasisi inayokaguliwa itakayoainisha hoja za ukaguzi pamoja na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa majibu na vielelezo kuhusiana na ripoti hiyo kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.
9. Kufuatilia majibu ya hoja za ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ili kuweza kujiridhisha na majibu ya hoja hizo.

10. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya mwisho kwa taasisi zinazokaguliwa inayoonesha hoja za ukaguzi zilizotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ambazo hazikupata majibu yenye kuridhisha kutokana na hoja zilizotolewa.
11. Kutoa ripoti kuu ya mwaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

## 1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka na kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na kufanikiwa kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbali mbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

## 1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI

Tunatoa shukurani za dhati kwa wenyeviti na wajumbe wa kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zao wanazochukuwa kusimamia uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yao kwa sekta mbali mbali.

Kamati za Baraza la Wawakilishi ni muhimu sana katika kuimarisha uwajibikaji na kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia. Kamati hizi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya Utawala Bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma.

Kutokana na umuhimu mkubwa wa Kamati za Baraza la Wawakilishi, Ofisi imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoanishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Aidha Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma (LAAC) inatoa mchango mkubwa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma na Kamati hii imekuwa ikishirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu katika kufuatilia ripoti zake na kutoa ushauri na mapendekezo mbali mbali kwa Serikali kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa matumizi ya rasilimali hizo kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Maelekezo, ushauri, maoni na michango inayotolewa na Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Baraza la Wawakilishi yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma na kuongezeka kwa ufanisi na tija katika utekelezaji wa mipango ya Serikali na kupelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla.

## 1.6 SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani kwa wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi ya mwaka 2019/2020.

Nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazozichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarisha utawala bora nchini.

Natoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali zinazochukuliwa katika kuimarisha Ofisi hii kiutendaji na watendaji kwa ujumla. Vile vile napenda kuwapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa juhudi zao wanazochukuwa hadi kufanikisha kukamilika kwa ripoti hii kwa wakati.

Aidha, ninawashukuru viongozi na watendaji wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watendaji wa taasisi mbali mbali za Serikali kwa mashirikiano mazuri wanayotupa wakati wa kutekeleza kazi zetu za ukaguzi.

........................................

**Dkt. OTHMAN ABBAS ALI**

**KAIMU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**ZANZIBAR**

# SURA YA PILI

## 2.0 HATI ZA UKAGUZI

## 2.1 UTANGULIZI

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hivyo, kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

## 2.2 AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

### 2.2.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika.

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuvuta umakini wa wasomaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija atatoa **Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo**.

Aya hii itawekwa tu pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa kwa kiasi kikubwa na inatakiwa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za hesabu pekee.

### 2.2.2 Hati Zisizoridhisha

Hati hizi hutolewa pale ambapo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zimeshindwa kuthibitishwa kutokana na athari zilizobainika na hivyo kupelekea taarifa hizo kutoonesha sura sahihi na halisi. Baadhi ya hati zilizotolewa katika kundi hili ni kama inavyoonekana hapo chini.

### (i) Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale (a) mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuhitimisha ukaguzi na kuona athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha; au (b) mkaguzi anapokuwa ameshindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumuwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho kwa ujumla wake si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha.

### (ii) Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

### (iii) Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa za fedha hizo.

## 2.3 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya hati za ukaguzi kumi (10) zimetolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi. Kati ya hati kumi zilizotolewa taasisi mbili (2) zimepata Hati zinazoridhisha , taasisi saba (7) zimepata Hati zenye shaka na taasisi moja (1) imepata Hati mbaya kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020.

Mchanganuo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 1: Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Mjini | Hati yenye shaka |
| 2. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | Hati yenye shaka |
| 3. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | Hati yenye shaka |
| 4. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" | Hati mbaya |
| 5. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" | Hati yenye shaka |
| 6. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | Hati inayoridhisha |
| 7. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Hati yenye shaka |
| 8. | Ruzuku | Baraza la Mji Chake Chake | Hati yenye shaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Ruzuku | Baraza la Mji Mkoani | Hati yenye shaka |
| 10. | Ruzuku | Baraza la Mji Wete | Hati inayoridhisha |

## 2.4 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na kifungu namba 77 (1) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Sheria nambari 7 ya mwaka 2014 , Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa zitayarishe na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali umeimarika ambapo hesabu hizo zimewasilishwa kwa wakati kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 2: Uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020**

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **2018/2019** | **2019/2020** |
| 1. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Mjini | 26/09/2019 | 24/09/2020 |
| 2. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 30/09/2019 | 30/09/2020 |
| 3. | Ruzuku | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 30/09/2019 | 28/09/2020 |
| 4. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' | 27/09/2019 | 30/09/2020 |
| 5. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" | 20/9/2019 | 30/09/2020 |
| 6. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 30/09/2019 | 29/09/2020 |
| 7. | Ruzuku | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 29/09/2019 | 30/09/2020 |
| 8. | Ruzuku | Baraza la Mji Chake Chake | 25/09/2019 | 28/09/2020 |
| 9. | Ruzuku | Baraza la Mji Mkoani | 27/09/2019 | 25/09/2020 |
| 10. | Ruzuku | Baraza la Mji Wete | 23/09/2019 | 23/09/2020 |

# SURA YA TATU

## 3.0 UANZISHWAJI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kusogeza huduma za jamii kwa wananchi katika sekta mbali mbali ambapo baadhi ya sekta zimegatuliwa kutoka Serikali Kuu na kupewa Mamlaka ya kuendesha shughuli mbali mbali za kutoa huduma za jamii kwa wananchi zikiwemo Sekta ya Elimu, Sekta ya Afya na Sekta ya Kilimo.

## 3.1 KUANZISHWA KWA MAMLAKA KWA MUJIBU WA SHERIA

Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa sheria namba 7 ya mwaka 2014. Mamlaka ya Serikali za Mitaa inapaswa kufuata Sheria namba 7 ya mwaka 2014 pamoja na sheria nyenginezo.

Katika kutekeleza majukumu yake Serikali za Mitaa zinawajibika kufanya kazi zake kwa kufuata sheria mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo Sheria ya usimamizi wa fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011.

## 3.2 LENGO LA KUANZISHWA KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa madhumuni ya kusogeza huduma kwa wananchi ili kuleta ufanisi wa utowaji huduma za Serikali, katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinasimamiwa na Mabaraza ya Madiwani ambao ndio wanaoidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya mamlaka hizo. Uendeshwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unasimamiwa na Wakurugenzi ambao ndio Maafisa Wahasibu na ndio wenye jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuidhinisha matumizi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

## 3.3 UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Ukaguzi wa hesabu ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya Ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa za fedha zitakazotayarishwa zitaonyesha sura halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo.

Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulifanywa kwa kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 2014, Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011 pamoja na Sheria nyenginezo.

Aidha ukaguzi uliangalia ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani, ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa mali za umma pamoja na mifumo ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa kiwango cha wastani katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kiwango hicho kimepelekea kubainika dosari mbali mbali ambazo zimewasilishwa kwa Maafisa Wahasibu kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na kufanyiwa marekebisho kwa hoja za ukaguzi zilizobainika. Aidha baadhi ya hoja za ukaguzi hazikuweza kurekebishwa kutokana na kutokupatika kwa vielelezo vinavyo husiana na hoja hizo.

# SURA YA NNE

## 4.0 MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## 4.1 BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ZANZIBAR

Tumekamilisha ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Manispaa ya Mjini kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, ukaguzi huo umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Manispaa ya Mjini pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini.

**Taarifa ya mapato**

Baraza la Manispaa Mjini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 17,205,557,546. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 4,775,400,000 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 12,430,157,546 ikiwa ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.
Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 16,362,034,020.12 zilikusanywa sawa na asilimia 95 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 3,953,050,542 ni kutoka vyanzo vya mapato vya baraza na jumla ya shilingi 12,408,983,478.12 ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.

**Taarifa ya matumizi**

Baraza la Manispaa Mjini katika mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 17,205,557,546. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 16,432,939,291 zilitumika sawa na asilimia 96 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.1.1 Kitengo cha ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit)

Kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu nambari 117 inaitaka kila taasisi ya Umma kuanzisha kitengo cha Ukaguzi wa ndani ambacho ni imara na madhubuti kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani.

Baraza la Manispaa ya Mjini limeanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya usimamizi wa fedha za umma, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa kitengo cha ukaguzi wa ndani kina mkaguzi mmoja tu hali ambayo inaweza kupelekea ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani kushindwa kufikiwa.

Kuwepo kwa Mkaguzi wa ndani mmoja katika kitengo cha ukaguzi wa ndani kunaweza kupelekea ufanisi mdogo wa kitengo cha ukaguzi wa ndani kushindwa kufikiwa

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya mjini kufanya jitihada za kuomba wakaguzi wa ndani kutoka Wizara ya fedha kwa ajili ya kuimarisha kazi za ukaguzi wa ndani za Baraza la Manispaa ya Mjini.

### 4.1.2 Kamati ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 kinaitaka kila taasisi ya Umma kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani kwa ajili ya kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani.

Baraza la Manispaa ya Mjini limeanzisha Kamati ya ukaguzi kwa mujibu wa kifungu namba 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka 2019/2020 kamati hiyo imefanya kikao kimoja.

Kutofanya kazi kwa kamati ya ukaguzi ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma sheria nambari 12 ya mwaka 2016, aidha inaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kurekebishwa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuweka utaratibu wa kuhakikisha Kamati ya ukaguzi inakutana kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za Umma sheria nambari 12 ya mwaka 2016.

### 4.1.3 Kukosekana kwa vitabu 300 vya Mapato ya Maegesho

Baraza la Manispaa Mjini linakusanya mapato ya maegesho katika maegesho yake mbali mbali. Ukaguzi umebaini kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato ya maegesho, hivyo mapato yaliokusanywa kupitia vitabu hivyo hayakuweza kukaguliwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Uchambuzi wa vitabu vilivyokosekana kwa ukaguzi ni kama vinavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 3: Vitabu vya stakabadhi vilivyokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Tarehe | Mtiririko wa nambari za stakabadhi | Jumla ya Vitabu | Aliyekabidhiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 8/7/2019 | 196001-197000 | 10 | Bakari Juma |
| 2 | 8/7/2019 | 197001-19800 | 10 | Bakari Juma |
| 3 | 8/7/2019 | 198001-19900 | 10 | Rehema Khamis |
| 4 | 8/7/2019 | 19900-20000 | 10 | Rehema Khamis |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | 10/7/2019 | 0001-1000 | 10 | Ussi Sleman |
| 6 | 10/7/2019 | 1001-2000 | 10 | Ussi Sleman |
| 7 | 10/7/2019 | 2001-3000 | 10 | Ussi Sleman |
| 8 | 10/7/2019 | 30001-4000 | 10 | Bakari Juma |
| 9 | 11/7/2019 | 4001-5000 | 10 | Rehema Khamis |
| 10 | 12/7/2019 | 5001-6000 | 10 | Ussi Sleman |
| 11 | 12/7/2019 | 6001-7000 | 10 | Ussi Sleman |
| 12 | 12/7/2019 | 7001-8000 | 10 | Ussi Sleman |
| 13 | 15/7/2019 | 8001-9000 | 10 | Ussi Sleman |
| 14 | 15/7/2019 | 9001-10,00 | 10 | Ussi Sleman |
| 15 | 19/7/2019 | 10001-1100 | 10 | Rehema Khamis |
| 16 | 19/7/2019 | 13001-14000 | 10 | Ussi Sleman |
| 17 | 24/7/2019 | 15001-1600 | 10 | Ussi Sleman |
| 18 | 24/7/2019 | 16001- 7000 | 10 | Ussi Sleman |
| 19 | 25/7/2019 | 18001-19000 | 10 | Rehema Khamis |
| 20 | 29/7/2019 | 21001-22000 | 10 | Ussi Sleman |
| 21 | 29/7/2019 | 22001-230001 | 10 | Rehema Khamis |
| 22 | 1/8/2019 | 23001-24000 | 10 | Rehema Khamis |
| 23 | 2/8/2019 | 26001-27000 | 10 | Ussi Sleman |
| 24 | 5/8/2019 | 27001-2800 | 10 | Rehema Khamis |
| 25 | 6/8/2019 | 28001-29000 | 10 | Ussi Sleman |
| 26 | 6/8/2019 | 29001-30000 | 10 | Ussi Sleman |
| 27 | 6/8/2019 | 30001-31000 | 10 | Ussi Sleman |
| 28 | 9/8/2019 | 31001-32000 | 10 | Ussi Sleman |
| 29 | 9/8/2019 | 34001-3500 | 10 | Rehema Khamis |
| 30 | 15/8/2019 | 37001-8300 | 10 | Ussi Suleman |
| **Jumla** | | | **300** | |

### 4.1.4 Vitabu vya stakabadhi ambavyo havikurikodiwa katika daftari la kutunzia stakabadhi (Counter Foil Register)

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Mjini limekusanya mapato kupitia vitabu vya stakabadhi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokurikodiwa kwa vitabu vya mapato katika daftari la kutunzia vitabu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha inaboresha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu ili kuweza kusawazisha dosari hiyo kwa kuingiza taarifa za mapato yaliyokusanywa kupitia stakabadhi hizo katika daftari la kutunzia mapato.

Uchambuzi wa vitabu ambavyo havikurikodiwa katika daftari la kutunzia stakabadhi ni kama vinavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 4: Vitabu vya stakabadhi ambavyo havikurikodiwa katika daftari la kutunzia stakabadhi**

| Namba | Tarehe | Mtiririko wa nambari za stakabadhi |
|---|---|---|
| 1. | 27/8/2019 | 64201-64300 |
| 2. | 27/8/2019 | 69501-69600 |
| 3. | 27/8/2019 | 42801-42900 |
| 4. | 3/7/2019 | 64801-64900 |
| 5. | 3/7/2019 | 65301-65400 |
| 6. | 3/7/2019 | 69401-69500 |
| 7. | 3/7/2019 | 69101-69200 |
| 8. | 3/7/2019 | 69001-70001 |
| 9. | 8/7/2019 | 69701-69789 |
| 10. | 9/7/2019 | 69001-69100 |

### 4.1.5 Vitabu vya mapato mengineyo ambavyo havijapatikana kwa ukaguzi

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Mjini limekusanya mapato kwa kutumia vitabu mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokupatikana kwa vitabu vya mapato mengineyo kwa ajili ya ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha unaboresha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu ili kuweza kusawazisha dosari hiyo.

Uchambuzi wa vitabu hivyo kama unaonyoonekana katika jadweli lifuatalo;

**Jadweli Nambari 5: Vitabu vya stakabadhi ambayo havikupatikana kwa ukaguzi**

| Namba | Tarehe | Mtiririko wa nambari za stakabadhi | Jumla ya Vitabu | Aliyekabidhiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 26/6/2019 | 119851-120000 | 3 | SAID RASHID |
| 2. | 2/7/2019 | 120001-120100 | 2 | USSI SULEIMAN |
| 3. | 5/7/2019 | 120101-120350 | 5 | SAID RASHID |
| 4. | 22/7/2019 | 120551-120600 | 1 | REHEMA KHALFAN |
| 5. | 30/07/2019 | 120651-120900 | 5 | SAID RASHID |
| 6. | 29/8/2019 | 128151-128300 | 3 | SAID RASHID |
| 7. | 2/9/2019 | 128301-128400 | 2 | SAID RASHID |
| 8. | 6/9/2019 | 128651-128900 | 5 | SAID RASHID |
| 9. | 10/9/2019 | 129051-129100 | 1 | USSI SULEIMAN |
| 10. | 19/12/2019 | 130701-130800 | 2 | SAID RASHID |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | 19/12/2019 | 131001-131050 | 1 | LAILAT ABDALLA |
| 12. | 19/12/2019 | 131101-31150 | 1 | ASHA SOUD |
| 13. | 23/12/2019 | 131151-131200 | 1 | REHEMA KHALFAN |
| 14. | 6/1/2020 | 131751-131800 | 1 | LAILAT ABDALLA |
| 15. | 28/1/2020 | 136101-136150 | 1 | LAILAT ABDALLA |
| 16. | 5/2/2020 | 142751-142800 | 1 | MIZA JUMA |
| 17. | 25/06/2020 | 171551-171600 | 1 | MWANAISHA ALI |
| 18. | 25/6/2020 | 171601-172000 | 8 | JUMA MAULID |
| **Jumla** | | | **44** | |

### 4.1.6 Kukosekana kwa mapato ya ukodishwaji wa bustani ya Jamhuri Garden shilingi 7,200,000

Baraza la Manispaa ya Mjini limeingia mkataba na Bi. Asya Moh'd Bafadhili kwa ajili ya ukodishwaji wa eneo la bustani ya Jamhuri (Jamhuri Garden) kuanzia tarehe 01/11/2010 hadi 31/10/2018 kwa gharama ya malipo ya shilingi 100,000 kwa kila mwezi.

Ukaguzi umeshindwa kupata uthibitisho wa makusanyo ya jumla ya shilingi 7,200,000 ambazo ni kodi ya eneo hilo kwa muda wa miaka sita kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2020. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba huo pamoja na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuupitia upya mkataba huo na kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba huo.

### 4.1.7 Dosari katika Zabuni ya Maegesho

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini limeingia Mkataba na kampuni ya Econex mkataba wenye nambari UMC/PPPs/NCS/04/2019 kwa ajili ya kazi ya wakala wa kutoa huduma ya ukusanyaji wa ada za maegesho kwa muda wa miaka mitatu kuanzia tarehe 09/08/2019 hadi tarehe 01/09/2022.

Aidha, katika makubaliano hayo dosari mbali mbali zimebainika ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za manunuzi katika kumtafuta wakala wa ukusanyaji wa mapato hayo kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi ulifanya tahthmini ya uwezo wa Baraza la Manispaa ya Mjini katika ukusanyaji wa mapato ya maegesho kutokana na taarifa za makusanyo ya mwaka wa fedha 2018/2019, Baraza la Manispaa mjini lilikusanya jumla ya shilingi 807,323,500 na tathmini iliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imebainika kampuni ya Econex ilikusanya jumla ya shilingi 560,276,914 kukiwa na upungufu wa jumla ya shilingi 247,046,586 ukilinganisha na fedha iliyokusanywa na kampuni ya Econex kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hivyo ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa ya Mjini lina uwezo wa kukusanya mapato makubwa zaidi ikiwa litaongeza jitihada na usimamizi mzuri wa mapato kuliko kuingia mkataba na kampuni hiyo jambo ambalo linaweza kupelekea kupotea kwa makusanyo ya mapato na kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya Upembuzi Yakinifu juu ya uwezo wa Baraza katika kukusanya mapato ya maegesho ili kuhakikisha Baraza linapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za Umma.

### 4.1.8 Kukosekana kwa mikataba ya ukodishaji maduka 85 masokoni

Baraza la Manispaa ya Mjini limefanya ujenzi wa maduka themanini na tano (85) katika maeneo ya masoko yaliyo katika Manispaa ya Mjini. Ukaguzi umeshindwa kupata mikataba ya maduka hayo wakati wa ukaguzi.

Kukosekana kupatikana kwa makubaliano ya mikataba kumepelekea ukaguzi kushindwa kuona makubaliano ya malipo pamoja na taratibu za kulipana.

Ukaguzi unapendekeza Baraza la Manispaa Mjini kufuata Sheria na taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha dosari iliyobainika inapatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria na taratibu.

Mchanganuo wa maduka hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 6: Maduka ambayo mikataba ya ukodishwaji wake haikupatikana kwa ukaguzi**

| Namba | Jina la Mfanya biashara | Anuani ya Soko | Idadi ya maduka |
|---|---|---|---|
| 1 | Hamad Yahya | Mombasa | 23 |
| 2 | Hamad Yahya | Mwanakwerekwe | 35 |
| 3 | Khamis Kizinga | Mwanakwerekwe | 9 |
| 4 | Salum Tom | Mwanakwerekwe | 18 |

### 4.1.9 Vitabu 79 vya ukusanyaji wa mapato ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi

Baraza la Manispaa Mjini kupitia Divisheni ya michirizi inakusanya mapato ya huduma ya usafishaji wa michirizi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokupatikana vitabu 79 vya kukusanyia mapato. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha inaboresha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu ili kuweza kusawazisha dosari hiyo.

Mchanganuo wa vitabu vya stakabadhi ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1.**

### 4.1.10 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 33,674,900

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Mjini limefanya malipo ya shilingi 33,674,900 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 7: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi ya malipo | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 46/10, 8/10/2019 | 4632 | BARAZA LA MANISPAA | 1,470,000 | Ikiwa ni Malipo ya posho la kujikimu |
| 2 | 60-62/10, 11/10/2019 | 4643 | ABDULSALAAM BUILDING LTD | 7,354,900 | Ikiwa ni Malipo kwa ajili ya usukumaji wa taka kwa kutumia kijiko |
| 3 | 50/11, 7/11/2019 | TT | SHIRIKA LA UMEME | 3,900,000 | Ikiwa ni Malipo kwa ajili ya ununuzi wa umeme kwa mita za mji mkongwe na barabarani |
| 4 | 55/8, 6/8/2019 | 4410 | KILIMANI CITY COOPERATIVE | 2,450,000 | Ikiwani Malipo yaliolipwa baada ya kukamilisha kazi |
| 5 | 40/02, 24-02-2020 | 4892 | BARAZA LA MANISPAA | 2,500,000 | Marejesho ya fedha zilizotumika kwa, ,shughuli mbalimbali |
| 6 | 101/3, 9/3/2020 | TT | ZANZIBAR PETROLEUM LTD | 16,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mafuta ya Disel lita 29,759 kwa magari ya tak ya manispaa |
| **Jumla** | | | | **33,674,900** | |

### 4.1.11 Matumizi yaliyotumika kinyume na mpango wa manunuzi shilingi 15,632,250

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Mjini lilifanya matumizi jumla ya fedha shilingi 15,632,250 zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa gari na vifaa kwa ajili ya Wadi ya Sogea.

Ukaguzi umebaini manunuzi hayo hayakupangwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa Baraza la Manispaa ya Mjini. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unapendekeza Baraza la Manispaa Mjini kufuata Sheria na taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha dosari iliyobainika inapatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria na taratibu hizo, ikiwemo kufanya manunuzi kwa mujibu wa mpango wa manunuzi.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 8: Malipo yaliyofanyika bila kuzingatia Mpango wa Manunuzi**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Jumla ya fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 27/07, 30-07-19 | 4361 | 10,450,000 | VISIWANI GENERAL SUPPLIER | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa gari (Town Hiace) Kwa wadi ya sogea |
| 2 | 46/09, 6/9/2019 | 4472 | 5,182,250 | R & F GENERAL SUPPLIER COMPANY | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya Wadi |
| **Jumla** | | | **15,632,250** | | |

### 4.1.12 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara shilingi 145,921,506

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa ya Mjini linakusanya mapato ya minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo jumla ya shilingi 145,921,506 zilikusanywa. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Baraza la Manispaa ya Mjini ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa ambayo sawa na shilingi 58,368,602 na asilimia 60 inawasilishwa Baraza la Manispaa Mjini ambayo sawa na shilingi 87,552,904.

Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Manispaa ya Mjini, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Baraza la Manispaa ya Mjini ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya Upembuzi Yakinifu (Feasibility study) ili kuhakikisha Baraza linapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabunina kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 9 : Makusanyo ya fedha za mapato yatokanayo na minara**

| Namba | Mwezi husika | Mapato yaliyokusanywa (SHS) | Gawio la mapato, asilimia 40 (SHS) | Gawio la mapato, asilimia 60 (SHS) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Machi, 2020 | 64,574,340 | 25,829,736 | 38,744,604.00 |
| 2. | April, 2020 | 60,000,000 | 24,000,000 | 36,000,000.00 |
| 3. | Mei, 2020 | 15,567,166 | 6,226,866 | 9,340,299.60 |
| 4. | Juni, 2020 | 5,780,000 | 2,312,000 | 3,468,000.00 |
| **Jumla** | | **145,921,506** | **58,368,602** | **87,552,903.60** |

## Maoni ya Ukaguzi

## Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Manispaa ya Mjini imepata Hati Yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.2 BARAZA LA MANISPAA YA WILAYA YA MAGHARIBI "A"

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Manispaa la Wilaya ya Magharibi "A" kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Matokeo ya ukaguzi huo yanatokana na kukagua kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Manispaa ya Wilaya ya Magharibi "A" pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza la Manispaa ya Wilaya ya magharibi "A".

**Taarifa ya mapato**

Baraza la Manispaa la Wilaya ya Magharibi "A" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,000,000,000 kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza.
Hadi kufikia 30 Juni 2020 jumla ya shilingi 1,227,991,234 zilikusanywa kutoka vyanzo vya mapato yya Baraza sawa na asilimia 100.9.

**Taarifa ya matumizi**

Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" katika mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,617,154,470.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 9,974,736,974 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 105 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.2.1 Kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato

Ukaguzi umebaini baraza la Manispaa ya Magharibi "A" limekusanya mapato kwenye vitengo mbali mbali vya kukusanyia mapato ya Baraza lakini vitabu vya stakabadhi vilivyotumika kukusanyia mapato hayohavikupatikana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 aidha kunapelekea kushindwa kujua mapato halisi yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo.

Mchanganuo wa orodha ya vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 2**.

### 4.2.2 Tofauti ya shilingi 1,526,123,819 iliyojitokeza katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka

Ukaguzi ulipitia taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na daftari la kutunzia fedha ili kuangalia uwiano kati ya taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka na daftari la kutunzia kumbu kumbu za mapato na matumizi ya Baraza la Manispaa ya Magharibi "A".

Ukaguzi umebaini jumla shilingi 11,310,574,959 ni matumizi yaliyoonekana kutumika kwenye daftari la kutunzia fedha kupitia hesabu ya Baraza la Manispaa Wilaya ya Magharib "A", aidha jumla ya shilingi 9,784,451,140 ni matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka, hivyo kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 1,526,123,819.

Kutoripotiwa hesabu sahihi katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa hiyo kutokuonyesha uhalisia kwa mujibu wa viwango vya utayarishaji wa taarifa za fedha. Aidha kunaweza kupelekea taarifa za hesabu za Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kutoonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016**.**

### 4.2.3 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 47,266,200

Ukaguzi umebaini Baraza la Manisapaa Wilaya ya Magharibi "A" imefanya malipo ya shilingi 47,266,200 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume namba 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 10 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Alielipwa | Jumla ya fedha (SH) | Maelezo ya Malipo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 19/8, 18/09/2019 | 1242 | Jayson Industry | 3,764,200 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununzi wa vifuko pamoja na neti nyeusi kwa ajili ya kitalu cha Mwera |
| 2 | 24/9/2019 | TT | Tusiyumbishane Cooperation | 2,017,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya gawio la makusanyo ya ushirika wa Tusiyumbishane Cooperation katka Diko la Kihinani |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | 36/9, 27/09/2019 | 1264 | Zan Clean Group | 2,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Malipo ya kikundi vya usafi |
| 4 | 34/09, 27/10/2019 | 1259 | Hakuna Mkamilifu | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo ya vikundi vya usafi |
| 5 | 47/9, 27/09/2019 | 1264 | Zan Clean Group | 2,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Malipo ya kikundi vya usafi |
| 6 | 22/6, 29/6/2020 | 1685 | Zanclean | 2,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 7 | 23/6, 29/6/2020 | | Hakuna Mkamilifu | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 8 | 33/3, 25/3/2020 | 1631 | Baraza la Manispaa Magharibi A | 4,880,000 | Ikiwa ni malipo ya kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ofisi. |
| 9 | 30/8, 28/8/2019 | 1207 | Zan Clean Group | 9,805,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi cha ZANCLEAN GROUP |
| 10 | 2/13, 13/2/2020 | 1585 | Baraza La Manispaa Magharibi A | 2,500,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 11 | 14/2, 13/2/2020 | 1586 | Baraza La Manispaa Magharibi A | 1,000,000 | Malipo ya Fedha kwa ajili yaMsaada kwa mwandishi wa habari wa Wilaya |
| 12 | 1/12, 14/1/2020 | 1449 | Baraza La Manispaa Magharibi A | 6,800,000 | Ikiwa ni Malipo ya fedha kwa ajili ya kikao cha Baraza la Manispaa |
| 13 | 1/8, 8/1/2020 | 1443 | Urban West Region | 5,000,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbaali ya Mkoa ya Shamrashamra za kilele cha sherehe za Mapinduzi |
| **Jumla** | | | | **47,266,200** | |

### 4.2.4 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 42,879,500

Ukaguzi umebaini Baraza la Manisapaa Wilaya ya Magharibi "A" limefanya malipo ya shilingi 42,879,500 kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa hati za malipo husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume naSheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 11: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 93/9, 13/09/2019 | 1225 | Mohd Fereji | 2,582,000 |
| 2 | 9I/9, 13/09/2019 | 1232 | Rajab Dadi | 3,906,000 |
| 3 | 23/9, 17/09/2019 | 1248 | Hassan Sons | 2,328,000 |
| 4 | 10-Jul | 1272 | B M M A | 7,980,800 |
| 5 | 19/10 | 1286 | Hamju Constru | 8,703,000 |
| 6 | 49/10 | 1322 | B M M A | 6,975,000 |
| 7 | 35/8 | 1211 | BMMA | 4,840,000 |
| 8 | 17/8 | 1193 | Zan Link | 4,100,000 |
| 9 | 14/7, 14/7/2019 | 1165 | Msa Auto Part | 1,464,700 |
| **Jumla** | | | | **42,879,500** |

### 4.2.5 Kukosekana kwa mikataba ya watoa huduma shilingi 19,000,000

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "A" imefanya malipo ya shilingi 19,000,000 kwa ajili ya kulipia huduma kutoka kwa wasambazaji wa huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba kati ya wasambazaji hao na Baraza la Manispaa ya Magharibi "A". Kufanya malipo kwa wasambazaji wa huduma bila ya kuwa na Mikataba kunapelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 12: Watoa huduma ambao hawana mikataba**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (SH) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/5, 3/1/2020 | 1439 | 2,500,000 | Zan Clean group | Malipo ya fedha kwa ajili ya Kikundi cha Zanclean Group |
| 2 | 5/3, 6/3/2020 | 1604 | 2,500,000 | Zan Clean Group | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 3 | 6/3, 6/3/2020 | 1605 | 2,000,000 | Hakuna Mkamilifu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 4 | 17/3, 13/3/2020 | 1618 | 5,000,000 | Zanlink | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uungaji wa huduma ya Internet |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | 4/4, 9/4/2020 | 1515 | 2,000,000 | Hakuna Mkamilifu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 6 | 6/4, 9/4/2020 | 1518 | 2,500,000 | Zan Clean Group | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| 7 | 22/4, 29/4/2020 | 1535 | 2,500,000 | Zan Clean Group | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi. |
| **Jumla** | | | **19,000,000** | | |

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Yenye Shaka**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" limepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.3 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Matokeo ya ukaguzi huo yanatokana na kukagua kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B".

**Taarifa ya mapato**

Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,100,000,000 kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza.
Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 1,940,169,299.45 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" sawa na asilimia 92.4 ya makadirio.

**Taarifa ya matumizi**

Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" katika mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 11,819,090,274.

Hadi kufikia 30Juni, 2020 jumla ya shilingi 11,354,907,446.25 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 96 ya makadirio.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.3.1 Kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato

Ukaguzi umebaini baraza la Manispaa ya Magharibi "B" limekusanya mapato kwenye vitengo mbali mbali vya kukusanyia mapato ya Baraza lakini vitabu vya stakabadhi vilivyotumika kukusanyia mapato hayo havikupatikana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 aidha kunapelekea kushindwa kujua mapato halisi yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo. Mchanganuo wa stakabadhi za vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 3.**

### 4.3.2 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara shilingi 78,174,340.34

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" linakusanya mapato ya minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo jumla ya shilingi 78,174,340.34 zilikusanywa. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa ambayo sawa na shilingi 29,469,736.00 na asilimia 60 inawasilishwa Baraza la Manispaa Magharibi "B" ambayo sawa na shilingi 46,904,604.20.

Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Manispaa ya Mjini, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Baraza la Manispaa ya Mjini ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya Upembuzi Yakinifu (Feasibility study) ili kuhakikisha Baraza linapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabunina kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

Mchanganuo wa mgawanyo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 13: Mgawanyo wa fedha za mapato ya Minara**

| Namba | Mwezi wa makusanyo | Jumla ya mapato yaliyokusanywa (Shs.) | Mapato ya Al-Jumra, asilimia 40 (Shs.) | Mapato ya Baraza la Manispaa, asilimia 60 (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Machi -2020 | 39,574,340 | 15,829,736 | 23,744,604 |
| 2 | Apr-20 | 5,000,000 | 200,000 | 3,000,000 |
| 3 | Mei-2020 | 30,000,000 | 12,000,000 | 18,000,000 |
| 4 | Juni-2020 | 3,600,000 | 1,440,000 | 2,160,000 |
| **Jumla** | | **78,174,340** | **29,469,736** | **46,904,604** |

### 4.3.3 Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 72,928,798

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa la Wilaya ya Magharibi "B" limefanya manunuzi ya vifaa mbalimbali venye thamani ya shilingi 72,928,798 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havijarikodiwa katika daftari la ghalani. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 14 : Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la ghalani**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha iliyolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 34/3, 12/3/2020 | 2338 | 4,000,000 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES CO LTD | Ikiwa ni malipo ya Zoezi la usafi na uzoaji wa taka katika majaa yasiyo rasmi na yaliyorasmi kupelekwa Kibele |
| 2 | 2/4, 8/4/2020 | 2433 | 5,631,068 | JAWALA AUTO PARTS | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa 1Pc Gear box machine Assy ya gari S M Z 368 B Fusso |
| 3 | 4/3, 1/4/2020 | 2415 | 3,160,194 | SULEIMAN ISMAIL | Ikiwa ni malipo kwa 350Pcs Matofali. 4Trip Mchanga mweupe |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 14/4, 3/4/2020 | 2426 | 8,525,000 | JUSTIDIA TRADERS | Ikiwa ni malipo kwa Ufukizaji wa dawa Vituo vya Afya Havijatajwa |
| 5 | 31/4, 15/4/2020 | 2447 | 4,582,524 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES CO LTD | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ufukizaji wa dawa katika majaa |
| 6 | 74/4, 27/4/2020 | 2497 | 5,882,353 | ABDULRAHMAN ISMAIL VUAI | Ikiwa ni malipo kwa Ununuzi wa 1Pc gear box engine Assy ya Z 347 FC |
| 7 | 72/3, 24/3/2020 | 2387 | 4,854,369 | ABDULSALAM BUILDING TZ LIMITED | Malipo ya kifusi Trip 14 kupitia Mfuko wa Maendeleo Wadi ya Fuoni. Kitaanzia njia tatu kwa Mashehe mpaka Birikani |
| 8 | 32/4, 15/4/2020 | 2448 | 12,671,990 | ABDULSALAM BUILDING TZ LIMITED | Ikiwa ni malipo ya Ununuzi na usambazaji wa kifusi katika Soko la Mombasa |
| 9 | 30/5 | 2522 | 4,500,000 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES | Ikiwa ni malipo ya marekebisho ya jengo la kituo cha afya magirisi kwa utiaji wa rangi ,kusafisha tarazo ,na upigaji wa vannish |
| 10 | 28/8, 9/8/2019 | | 3,800,000 | JAWABA AURO PARK | Ikiwa ni malipo ya deni la kwa gari iliyofanyiwa Over Hall SMZ 515 Fuso |
| 11 | 17/2, 29/1/2020 | 2270 | 1,940,000 | Skotch General Supplies CO ltd | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ukarabati wa madarasa matano pamoja na koridoo skuli ya chukwani. |
| 12 | 23/2, 11/2/2020 | 2282 | 4,370,000 | Skotch General Supplies CO ltd | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa kwa ajili ya matumizi ya kuanzisha shamba darasa la malishio ya mifugo shehia ya maungani. |
| 13 | 59/1, 22//1/2020 | 2204 | 4,161,300 | Abdulsalam Building tz ltd | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi skuli ya chekechea fumba (Wadi ya Maungani) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | 101/1, 28/1/2020 | 2260 | 4,850,000 | Adam Zuberi chande | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa kituo cha daladala mbweni |
| **Jumla** | | | **72,928,798** | | |

### 4.3.4 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 43,552,105

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa la Magharibi 'B' imefanya malipo ya shilingi 43,552,105 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 (1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli nambari 15: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 4/7, 7/7/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 3,472,500 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya safari ya kikazi nje ya nchi katika mafunzo ya muda mfupi |
| 2. | 21/7, 15/07/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,130,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya posho la safari |
| 3. | 58/7, 22/8/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B(FEDHA UCHUMI) | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa choo cha Kwale pamoja na uchukuzi wa matofali |
| 4. | 33/7, 29/7/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo ya watu wa bustani barabara ya Uwanja wa Ndege |
| 5. | 52/8, 22/08/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa choo cha kwale pamoja na uchukuzi wa matofali |
| 6. | 51/8, 21/08/2019 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 19,299,605 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya mashimo ya karo na kisima katiki kituo cha Afya Bwefumu pamoja na matengenezo ya nyumba ya daktari kituo cha afya Bwefum |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | 72/8,<br>28/8/2019 | BARAZA LA MANISPA MAGHARIBI B | 12,650,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi kwa kamati mbili,kamati ya fedha na kamati ya Mipango Miji. |
| **Jumla** | | | **43,552,105** | |

### 4.3.5 Kukosekana kwa mikataba shilingi 22,476,000

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa la Magharibi "B" imefanya malipo ya shilingi 22,476,000 kwa ajili ya kugharamia vikundi mbali mbali vya Usafi na Ulinzi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa Mikataba ya vikundi hivyo, ili kuweza kujiridhisha kiasi halisi cha malipo, muda na taratibu za malipo ya mikataba hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 16: Malipo yaliyofanyika bila ya mikataba**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 11/3,<br>2/3/2020 | TT | 2,000,000 | JUMUIYA YA KIKUNDI CHA TUMEFIKA | Malipo kwa ajili ya Kikundi cha Tumefika kwa Mwezi wa February 2020 |
| 2 | 59/3,<br>17/3/2020 | 2360 | 1,952,000 | SUBIRA MAKAME MUSSA | Malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi Shehia ya Pangawe |
| 3 | 4/01,<br>1/4/2020 | TT | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wa kikundi cha Mazingira Mombasa |
| 4 | 07/05,<br>27/4/2020 | 2498 | 3,000,000 | WAKALA WA ULINZI | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya ulinzi |
| 5 | 7/5 | 2498 | 3,000,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Huduma ya ulinzi |
| 6 | 25/03 | 2332 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Huduma ya ulinzi |
| 7 | 4/3 | 2295 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Huduma ya ulinzi |
| 8 | 5/6 | 2545 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Huduma ya ulinzi |
| 9 | 12/5 | 2505 | 1,440,000 | ZANZIBAR MODIFYING SECURITY SERVICE | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma ya ulinzi katika kampuni |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | 73/05 | TT | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA KWA MCHINA ZANZIBAR | Malipo kwa ajili ya posho wa vijana wa sokoni |
| 11 | 8/6 | TT | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA ZANZIBAR | Malipo kwa ajili ya posho wa vijana wa sokoni |
| 12 | 4/11 | TT | 1,784,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA ZNZ | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma za usafi |
| 13 | 2/11 | 2004 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Huduma ya ulinzi |
| **Jumla** | | | **22,476,000** | | |

### 4.3.6 Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao mikataba yao imeshamaliza muda shilingi 8,371,000

Ukaguzi umebaini kuwepo wa wafanyakazi wa mkataba ambao mikataba yao ishamaliza muda kisheria jambo ambalo linaweza kupelekea kuwakosesha haki zao za msingi pale ambapo linapojitokeza tatizo la kisheria ambalo litahusisha na namna ya uajiri wake. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011. Mchanganuo wa watumishi ambao mikataba yao imekwisha muda wake unaonekana katika **Kiambatisho Nambari 4.**

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Yenye Shaka**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" imepata Hati Yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.4 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "A"

Ukaguzi wa hesabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, ukaguzi huo umefanywa kwa kufuata sheria , kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri.

**Taarifa ya mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 649,225,700 kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 711,501,226 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri ikiwa sawa na asilimia 109 ya makadirio.

**Taarifa ya matumizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,257,876,867.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 7,971,806,679 zilitumika ikiwa ni sawa na asilimia 96 ya makadirio.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.4.1 Kamati ya ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016 inaitaka taasisi ya serikali kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani ili kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani wa ndani katika taasisi hiyo. Ukaguzi umebaini kuwa kamati ya ukaguzi ya Baraza la Mji la Wilaya ya kaskazini 'A' haijakaa kikao hata kimoja kwa lengo la kutathmini udhibiti wa ndani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016.

Kutofanya kazi kwa kamati ya ukaguzi ya Baraza la Mji la Wilaya ya Kaskazini "A" kunaweza kupelekea vihatarishi vya Halmashauri kutokubainika mapema na kunaweza kupelekea ukiukwaji wa sheria mbali mbali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji la Wilaya Kaskazini "A" kuhakikisha kamati ya ukaguzi inafanya kazi zake kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### 4.4.2 Dosari katika taratibu za manunuzi shilingi 116,230,000

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imefunga mkataba na Kampuni ya Trident Limited wenye gharama ya shilingi 116,230,000 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara ya Hamburu. Ukaguzi umebaini kutofuatwa kwa taratibu za kumtafuta mzabuni wa kazi hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, pamoja na kupelekea kufanyika kwa manunuzi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' kufanya manunuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 17: Malipo yaliyofanywa kwa Kampuni ya Trident Limited**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 23/5, 4/5/2020 | Trident Limited | 33,822,930 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Awamu ya kwanza kwa ajili ya Ukarabati wa barabara ya HAMBURU |
| 2 | 39/5, 29/4/2020 | Trident Limited | 38,123,440 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Awamu ya pili kwa ajili ya Ukarabati wa barabara ya HAMBURU |
| **Jumla** | | | **71,946,370** | |

### 4.4.3 Kutowasilishwa kwa fedha za makato katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii shilingi 174,000,000

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji la Wilaya ya Kaskazini "A" halikuwasilisha Michango ya jumla ya shilingi 174,000,000 ya wafanyakazi kwenda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa miezi miwili ya Disemba na Januari, fedha hizo zilizopaswa kulipwa zilitumika kwa ajili ya kazi nyengine za Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A". Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Sheria nambari 2 ya mwaka 2015.

Kutumia fedha zilizokatwa kwa ajili ya malimbikizo ya wafanyakazi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kutumika kwa matumizi mengineyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi wa Jamii nambari 2 ya mwaka 2015.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kuwasilisha Michango ya Wafanyakazi hao kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mara moja, ili kuweza kuendana na mfumo mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu za mikato ya wafanyakazi hao.

### 4.4.4 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" linakusanya mapato ya Minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo ukaguzi umeshindwa kuona kima halisi cha fedha kilichokusanywa na kampuni hiyo.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A". Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A", kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kima halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwaMkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Kukusanya mapato kupitia wakala wa ukusanyaji wa mapato ya minara kunapelekea Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kukosa mapato kwa kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" bila ya kumtumia wakala.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kufanya Upembuzi Yakinifu ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

### 4.4.5 Kukosekana kwa mikataba ya kazi za uzoaji wa taka shilingi 17,460,000

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imefanya malipo ya shilingi 17,460,000 kwa ajili ya kugharamia kazi za uzoaji wa taka za Halmashauri, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba ya uzoaji wa taka, ili kuweza kujiridhisha kiasi halisi cha makubaliano ya malipo, muda wa mkataba pamoja na taratibu za malipo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, pamoja na kutokupatikana tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kufuata Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa kufunga mikataba na watoaji huduma ili kuwepo kwa uwajibikaji katika utekelezaji wa kazi za Halmashauri. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 18: Malipo yaliyofanyika bila ya mikataba**

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (SH) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3/3, 20/03/2020 | 119 | ALI SALUM MCHENGA | 2,910,000 | Ikiwa ni malipoi kwa ajili ya uzoaji wa taka |
| 2 | 8/1, 23/01/2020 | 110 | Ali SALUM MCHENGA | 2,910,000 | Ikiwa ni malipoi kwa ajili ya uzoaji wa taka |
| 3 | 11/4, 9/4/2020 | 1885 | ALI SALUM MCHENGA | 2,910,000 | Ikiwa ni malipoi kwa ajili ya uzoaji wa taka Eneo la Kinyasini |
| 4 | 8/11, 13/11/2019 | 93 | ALI SALUM MCHENGA | 2,910,000 | Ikiwa ni malipoi kwa ajili ya uzoaji wa taka Eneo la Kinyasini |
| 5 | 6/11, 21/11/2019 | 108 | MHM ENTERPRISES | 1,164,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Uzoaji wa Taka eneo la kinyasini |
| 6 | 14/11, 21/11/2019 | 100 | MHM ENTERPRISES | 1,164,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Uzoaji wa Taka eneo la kinyasini |
| 7 | 5/10, 22/10/2019 | 83 | MHM ENTER-PRISES | 1,164,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Uzoaji wa Taka eneo la kinyasini |
| 8 | 2/9, 12/9/2019 | 77 | MHM ENTER-PRISES | 2,328,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Uzoaji wa Taka eneo la kinyasini |
| **Jumla** | | | | **17,460,000** | |

### 4.4.6 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 184,190,478

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imefanya malipo ya shilingi 184,190,478 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Halmashauri, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma sheria namba 12 ya mwaka2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 19: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 5/5, 13/05/2020 | TT | H/W/KA | 4,320,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 2. | 5/3, 20/03/2020 | 118 | SHARIF AMOUR BAKAR | 13,587,760 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Uzio wa eneo la Ofisi mpya |
| 3. | 5/2, 22/02/2020 | TT | H/W/K A | 59,120,019 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo |
| 4. | 9/1, 23/01/2020 | 111 | MOHAMMED RAJAB MOHAMMED | 1,131,020 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi vya fungurefu |
| 5. | 911, 14/11/2019 | 94 | Double Two GENERAL SUPPLY | 4,141,900 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya maji ya kisima cha skuli ya mlilile |
| 6. | 2/11, 1/11/2019 | 88 | KHAMIS JUMANNE MLEKWA | 9,700,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Minara minne ya fungurefu |
| 7. | 5/5, 13/05/2020 | TT | H/W/K A | 4,320,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 8. | 5/3, 20/03/2020 | 118 | SHARIF AMOUR BAKAR | 13,587,760 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Uzio wa eneo la Ofisi mpya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. | 5/2, 22/02/2020 | TT | H/W/K A | 59,120,019 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo |
| 10. | 2/1, 23/1/2020 | 1802 | HALMASHAURI YA WILLAYA YA KASKAZINI A | 2,340,000 | Ikiwa ni malipo ya kulipia gharama za wachukuzi na wasambazaji na boti kwenda Tumbatu kupeleka mabuku ya Skuli |
| 11. | 4/1, 17/1/2020 | 1804 | HALMASHAURI YA WILLAYA YA KASKAZINI A | 2,120,000 | Ikiwa ni malipo ya marejesho ya fedha za safari kwa ajili ya nauli kwa watumishi wa Halmashauri ya W/Kasskazini A |
| 12. | 12/1, 29/1/2020 | 1813 | DAWOOD TRADERS | 5,000,000 | Ikiwa ni malipo ya posho maalum kwa wafanyakazi walioshiriki katika Operesheni maalum ya usiku ya ukaguzi wa mazingira kwa muda wa siku 10 |
| 13. | 18/8, 23/8/2019 | | HALMASHAURI YA WILAYA KASKAZINI A | 5,702,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli sekta ya misitu kwa mwezi wa july(ikiwa ni ununuzi wa computer) |
| **Jumla** | | | | **184,190,478** | |

### 4.4.7 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari la ghalani shilingi 54,732,540

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imefanya matumizi ya jumla ya shilingi 54,732,540 kwa ajili ya manunuzi ya vifaa mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

## Jadweli Nambari 20 : Vifaa ambavyo havijarikodiwa ghalani

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 7/5, 11/5/2020 | 1902 | JECHA MBUGA | 9,674,780 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi wa vyoo skuli Tumbatu |
| 2. | 10/5, 13/05/2020 | 1906 | MUHALI COOPERATIVE | 5,238,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa CALVAT kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Donge |
| 3. | 12/5, 19/05/2020 | 1908 | MUHAMMAD BAKARI RAMADHANI | 3,880,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kodi ya AXCEVETAR Kwa ajili ya uchimbaji wa msingi wa Daraja eneo la Donge |
| 4. | 18/5, 22/05/2020 | 1915 | H/W/K/A | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ununuzi wa mawe na mchanga |
| 5. | 59/6, 30/06/2020 | TT | SHANGANI ENTERPRISES | 5,800,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa Honda moja ya ofisi |
| 6. | 56/6, 30/06/2020 | TT | KHAMIS JUMANNE MLEKWA | 5,200,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Tank 2 za maji |
| 7. | 9/6, 10/6/2020 | 1932 | KHAMIS JUMANNE MLEKWA | 8,075,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa matofali ya ujenzi wa skuli ya maandalizi chaani |
| 8. | 1/6, 1/6/2020 | 1921 | ABRAHMAN ISMAIL VUAI | 1,277,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya services ya magari ya Halmashauri |
| 9. | 5/3, 20/03/2020 | 118 | SHARIF AMOUR BAKAR | 13,587,760 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Uzio wa eneo la Ofisi mpya |
| **Jumla** | | | | **54,732,540** | |

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Mbaya**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazioneshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" imepata hati mbaya kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.5 HALMASHAURI YA WILAYA YAKASKAZINI "B"

Ukaguzi wa hesabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Matokeo ya ukaguzi huo yanatokana na kukagua kumbukumbu za hesabu za shughuli za Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B".

**Taarifa ya mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya shilingi 2,090,933,373 kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 1,263,389,912 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato ikiwa ni sawa na asilimia 60.4 ya makadirio.

**Taarifa za matumizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 6,869,733,373 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 6,414,575,696.49 zimetumika kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia 93 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.5.1 Kamati ya ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 kinaitaka kila taasisi ya Umma kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani kwa ajili ya kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" imeanzisha Kamati ya ukaguzi kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka 2019/2020 kamati hiyo imefanya kikao kimoja tu, jambo ambalo linaweza kupelekea dosari za kiutendaji kwa kutokurekebishwa kwa wakati kutokana na Kamati kushindwa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### 4.5.2 Vitabu vya stakabadhi ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa vitabu vya stakabadhi za malipo ya ukusanyaji mapato ya mazao ambavyo vimerikodiwa kwenye daftari la kutunzia kumbu kumbu za stakabadhi (Counterfoil Register) ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 30 (2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kusawazisha dosari hiyo kwa kutafutwa vitabu hivyo vya stakabadhi kwa ajili ya ukaguzi. Mchanganuo wa vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 21: Vitabu ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi**

| Namba | Nambari ya Kitabu | Aliyekabidhiwa |
|---|---|---|
| 1 | 110801-110900 | JUMA RAJAB AME |
| 2 | 104201-104300 | MUHAMED ALI AME |
| 3 | 104401-104500 | SLEMAN MWINYIDADI HAJI |
| 4 | 1045501-104600 | MUSTAFA HAJI ABDALLA |
| 5 | 105201-105300 | - |
| 6 | 105701-105800 | OMAR KHAMIS ABDALLA |
| 7 | 105901-10600 | ALHAJI BAKAR JUMA |
| 8 | 106701-100800 | MATINDE YATABU |
| 9 | 107401-107500 | SALEHE HAMIS IBRAHIM |
| 10 | 107501-107600 | MAKAME HUSSEN |
| 11 | 107601-107700 | MUSSA AKI KHAMIS |
| 12 | 107801-107900 | KHAMIS USSI MLINDE |
| 13 | 10901-108000 | ASHA HAJI KHAMIS |
| 14 | 108801-108900 | ALHAJI BAKAR JUMA |
| 15 | 108701-108800 | ABDALLA MASHANO HAJI |
| 16 | 108901-109000 | KHAMIS USSI MLINDE |
| 17 | 109101-109200 | ALI AMER KHAMIS |
| 18 | 109201-109300 | SUBEHA SHARIF SILIMA |

### 4.5.3 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara shilingi 131,936,140

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" inakusanya mapato ya minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo jumla ya shilingi 131,936,140 zilikusanywa. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa ambayo sawa na shilingi 52,774,456 na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" ambayo sawa na shilingi 79,161,684. Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata Wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B", kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kufanya Upembuzi yakinifu (Feasibility study) ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 22: Mgawanyo wa mapato ya minara**

| Mwezi wa makusanyo | Mwaka | Jumla ya mapato (Shs) | Mapato ya Al-jumra, asilimia 40(Shs.) | Mapato ya Halmashauri, asilimia 60 (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| Julai | 2019 | 90,000.0 | 36,000.0 | 54,000.0 |
| Agost | 2019 | 11,771,800.0 | 4,708,720.0 | 7,063,080.0 |
| Septemba | 2019 | 8,160,000.0 | 3,264,000.0 | 4,896,000.0 |
| October | 2019 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Novemba | 2019 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Disemba | 2019 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Januari | 2020 | 4,760,000.0 | 1,904,000.0 | 2,856,000.0 |
| Febuari | 2020 | 8,460,000.0 | 3,384,000.0 | 5,076,000.0 |
| Machi | 2020 | 41,194,340.0 | 16,477,736.0 | 24,716,604.0 |
| Aprili | 2020 | 35,000,000.0 | 14,000,000.0 | 21,000,000.0 |
| Mei | 2020 | 7,500,000.0 | 3,000,000.0 | 4,500,000.0 |
| Juni | 2020 | 15,000,000.0 | 6,000,000.0 | 9,000,000.0 |
| **Jumla** | | **131,936,140.0** | **52,774,456.0** | **79,161,684.0** |

### 4.5.4 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 64,388,579

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" imefanya malipo ya shilingi 64,388,579 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Halmashauri.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma sheria namba 12 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 23: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 59, 26/06/2020 | 32 | Mkurugenzi H/W/K B | 7,633,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya masurufu. |
| 2. | 62, 26/06/2020 | 314 | Freddy Decoration And Catering | 4,449,875 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 3. | 81, 29/06/2020 | 317 | Mkurugenzi H/W/K B | 1,800,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya masurufu |
| 4. | 86, 30/06/2020 | TT | Opportunity Tanzania Ltd | 1,873,648 | Malipo ya mikato ya wafanya kazi |
| 5. | 59, 26/06/2020 | 312 | Mkurugenzi H/W/K B | 7,633,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya masurufu. |
| 6. | 59, 26/06/2020 | 32 | Mkurugenzi H/W/K B | 7,633,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya masurufu |
| 7. | 26/10, 8/10/2019 | 77 | Mkurugenzi Halmashauri Kas B | 1,860,000 | ikiwa ni malipo kwa ajili ya kazi maalum. |
| 8. | 76/10, 24/10/2019 | TT | Platinum Crdit | 5,162,699 | ikiwa ni malipo kwa ajili ya mkato kwa wafanya kazi wanaokatwa na taasisi ya platinum credit bank |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. | 77/10, 24/10/2019 | TT | Elimu Saving And Credit | 9,660,657 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mkato wa Saving and Credit Zanzibar |
| 10. | 54/10, 21/10/2019 | 74 | Mkurugenzi Halmashauri Kas B | 1,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya msaada kuchapisha vitabu |
| 11. | 11/8, 06/8/20119 | 17 | Halmashauri Ya Wilaya Ya Kaskazini B | 3,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 12. | 28/08, 7/8/2019 | 20 | Halmashauri Ya Wilaya Ya Kaskazini B | 8,582,700 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 13. | 22/1, 6/1/2020 | 172 | Halmashauri Ya Wilaya Ya Kaskazini B | 1,600,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kodi ya gari na ununuzi wa Chakula. |
| 14. | 51/12, 12/31/2019 | 162 | Abdi Mbarouk Mo-hammed | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya Gari Escudo SMZ 505A. |
| **Jumla** | | | | **64,388,579** | |

### 4.5.5 Dosari Katika taratibu za manunuzi shilingi 218,347,200

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" imefunga mkataba na Kampuni ya Trident Limited wenye gharama ya shilingi 218,347,200 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kupitia miradi ya wadi. Ukaguzi umebaini kutofuatwa kwa taratibu za kumtafuta mzabuni wa kazi hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, pamoja na kupelekea kufanyika kwa manunuzi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji la Wilaya ya Kaskazini 'B' kufanya manunuzi kwa kuzingatia sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 24: Malipo yaliyofanywa kwa kampuni ya Trident Limited**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (SH) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 49/6, 22/06/2020 | TRIDENT | 10,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya muendelezo wa malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara miradi ya wadi |
| 2 | 1/6, 2/6/2020 | TRIDENT | 40,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya muendelezo wa malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara miradi ya wadi |
| 3 | - Ya 16/3/2020 | TRIEDENT LIMITED | 4,000,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kulipia gharama za uchongaji wa Barabara, kutawanya na kushindilia kifusi Manga Pwani |
| 4 | 34/3, 16/3/2020 | TRIEDENT LIMITED | 29,400,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya Kifusi kwa matumizi ya njia za ndani ya manga Pwani kwa awamu ya kwanza, tani 25 |
| **Jumla** | | | **83,400,000** | |

### 4.5.6 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari la ghalani shilingi 72,296,363

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" imefanya matumizi kwa ajili ya manunuzi ya vifaa mbalimbali dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani nikwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 25: Vifaa ambavyo havijarikodiwa ghalani**

| Nam | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 20/6, 8/6/2020 | 299 | ALLYM AUTO GARAGE | 1,748,000 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa vya magari |
| 2 | 30/4, 22/04/2020 | 276 | ASU TRADER AND GENERAL SUPPLIER | 7,017,178 | Ikiwa ni malipo ya utengenezaji wa madirisha kituo cha kitope |
| 3 | 64/6, 26/06/2020 | 316 | ZPRINT LIMITED | 1,050,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Uchapishaji wa vitabu vya Documentary |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 45/10, 11/10/2019 | 88 | SAYYID MUKY MAKAME | 5,058,065 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa rangi, vifaa vya maji,dongevijibweni na vifaa vya umeme. |
| 5 | 11/10, 8/10/2019 | 76 | UNGUJA PHAMACY | 24,105,470 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na vifaa vya usafi kutumika vituo vyya afya |
| 6 | 54/10, 21/10/2019 | 74 | MKURUGENZI HALMASHAURI KAS B | 1,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya msaada kuchapisha vitabu vya kusomeshea wagonjwa |
| 7 | 16/7, 16/07/2019 | TT | UNITED PETOLEUM | 5,180,200 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajil ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi. |
| 8 | 27/8, 7/8/2019 | TT | ABASI HAJI WAHAJI | 7,200,000 | Ikiwa ni alipo kwa ajili ya ununzi wa chakula |
| 9 | 75/2, 27/2/2020 | 233 | SAYYID MUKKY MAKAME | 3,283,450 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 10 | 30/12, 12/4/2019 | TT | SIDE PC EXPERT & RENOVATION | 12,319,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa komputa desktop, laptop na printer |
| 11 | 10/12, 12/4/2019 | 141 | MULT COLOR PRINTERS | 3,835,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uchapishaji leseni za video, leseni za biashara na fomu za maombi ya leseni |
| **JUMLA** | | | | **72,296,363** | |

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Yenye Shaka**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" imepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.6 HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI

Ukaguzi wa hesabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Halmashauri ya Wilaya ya Kati pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani (Internal Control) ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri.

**Taarifa ya mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,000,000,000 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Halmashauri ya Wilaya ya Kati ilikusanya jumla ya shilingi 1,246,130,521 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato ikiwa sawa na asilimia 124 ya makadirio.

**Taarifa ya matumizi**
Halmashauri ya Wilaya ya Kati ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,784,446,000 kwa kazi za kawaida Kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.
Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 8,717,958,654 zimetumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 99 ya makadirio.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.6.1 Kamati ya ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016 kinaitaka kila taasisi ya Umma kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani kwa ajili ya kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani.

Halmashauri ya Wilaya ya Kati imeanzisha Kamati ya ukaguzi kwa mujibu wa kifungu namba 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka 2019/2020 kamati imeshindwa kufanya vikao vyake kwa mujibu wa sheria.

Kutofanya kazi kwa kamati ya ukaguzi ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma sheria namba 12 ya mwaka 2016, aidha inaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kurekebishwa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati kuweka utaratibu wa kuhakikisha Kamati ya ukaguzi wa ndani inakutana kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### 4.6.2 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara shilingi 108,398,680.68

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kati inakusanya mapato ya minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo jumla ya shilingi 108,398,680.68 zilikusanywa. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Katiambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa ambayo sawa na shilingi 43,359,472 na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati ambayo sawa na shilingi 65,039,208.68.

Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwaMkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Katiambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kati kufanya Upembuzi yakinifu (Feasibility study) ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 26: Mgawanyo wa mapato ya minara**

| Namba | Tarehe | Jumla ya mapato yaliyokusanywa (Shs.) | Mapato ya Al-jumra, asilimia 40 (Shs.) | Mapato ya Halmashauri, asilimia 60 (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 18/3/2020 | 14,574,340.34 | 5,829,736 | 8,744,604.20 |
| 2. | 18/3/2020 | 58,324,340.34 | 23,329,736 | 34,994,604.20 |
| 3. | 24/3/2020 | 20,000,000.00 | 8,000,000 | 12,000,000.00 |
| 4. | 27/4/2020 | 8,000,000.00 | 3,200,000 | 4,800,000.00 |
| 5. | 8/5/2020 | 2,500,000.00 | 1,000,000 | 1,500,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | 8/5/2020 | 5,000,000.00 | 2,000,000 | 3,000,000.00 |
| **Jumla** | | **108,398,680.68** | **43,359,472** | **65,039,208.41** |

### 4.6.3 Dosari katika utayarishaji wa malipo shilingi 17,874,800

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati imefanya malipo ya shilingi 17,874,800 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Halmashauri, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo ya fedha kwa njia ya fedha taslimu (Cash Payment) badala ya kufanya malipo kwa kutumia hundi za benki, kufanya hivyo kunaweza kupelekea vihatarishi (Risk) katika utunzaji wa fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi waHalmashauri ya Wilaya ya Kati kufanya malipo kwa kutumia hundi za benki au kufanya uhaulishaji kupitia hesabu za kibenki ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 27: Malipo yaliyofanyika kwa njia taslim**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 48/6, 25/6/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,100,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ununuzi wa masufuria kwa skuli za maandalizi za Wilaya ya kati |
| 2. | 46/6, 23/06/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 5,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa fomu na viatu kwa polisi wa ha wil ya kati |
| 3. | 26/6, 8/6/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 628,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa Taizi katika Chumba cha kiti cha Meno Unguja Ukuu |
| 4. | 19/6, 5/6/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,146,800 | Ikiwa ni malipo kwa ajili matumizi ya ofisi |
| 5. | 10/6, 4/6/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 5,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili matumizi ya ofisi |
| 6. | 9/6, 4/6/2020 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 4,500,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili matumizi ya ofisi |
| **Jumla** | | | **17,874,800** | |

### 4.6.4 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 35,382,232

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati imefanya malipo ya shilingi 35,382,232 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Halmashauri.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wamalipo hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 28: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (Shs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 36/2, 26/2/2020 | 1813 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,000,000 | Ikwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa vyoo dunga kiem-beni na ujenzi wa kibanda cha maji |
| 2 | 16/1, 10/1/2020 | 146 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,700,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula na maji katika uzinduzi wa wa jengo la huduma za mama na mtoto |
| 3 | 32/1, 27/1/2020 | 158 | Zanzibar Petroleum | 3,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 4 | 1/8, 1/8/2019 | 1570 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununzi wa matofali |
| 5 | 1/8, 1/8/2019 | 1570 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununzi wa matofali |
| 6 | 15/11/2019 | TT | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 3,510,001 | ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya posho la waheshimiwa madiwani kwa mwezi wa octobar |
| 7 | 28/11, 19/11/2019 | 1468 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 7,000,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi kwa waheshimiwa madiwani pamoja na watendaji katika mji wa wa arusha pamoja na kukuza uhusiano wetu |
| 8 | 41/11, 13/11/2019 | TT | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 2,316,231 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kodi ya ZRB Kwa mwezi wa julai mpaka tisa 2019 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | 21/11, 15/11/2019 | 1466 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,260,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kumalizia ujenzi wa ofisi ya tawi wa la ccm uzi ng'ambwa ambao litafunguliwa na mweshimiwa RAIS |
| 10 | 24/11, 15/11/2019 | 1466 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 1,320,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa vijana wana-olala kambi katika ujenzi wa tawi la ccm uzi ngambwa |
| 11 | 26/11, 15/11/2019 | 1466 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 500,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa madereva walioshiriki katika ziara ya opokeaji mwenge na mbio za mwenge kwa mkoa wa kusini Unguja |
| 12 | 27/11, 11/15/2019 | 1467 | Hal-mashauri ya Wilaya ya Kati | 4,686,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 13 | 4/11, 11/9/2019 | 1462 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | 4,140,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya services ya gari za halimashauri ya wilaya ya kati |
| 14 | 15/11, 11/11/2019 | 1464 | Khamis Kassim Khamis | 2,950,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya upambaji wa siku ya kuadhimisha mwenge wa uhuru |
| **Jumla** | | | | **35,382,232** | |

## Maoni ya Ukaguzi

### Hati Inayoridhisha Yenye Aya ya Msisitizo

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Kati imepata Hati inayoridhisha yenye aya ya msisitizo kutokana na hoja zilizoainishwa hapo juu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.7 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Ukaguzi wa hesabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 umefanywa kwa kufuata sheria , kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri.

**Taarifa ya mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 240,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020, jumla ya shilingi 264,333,480 zilikusanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni sawa na asilimia 110 ya makadirio.

**Taarifa za matumizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,522,700,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 327,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 4,237,776,856 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 93.7 ya makadirio na shilingi 231,172,268 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 77.8 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.7.1 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 55,179,459

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shilingi 55,179,459 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za halmashauri.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

## Jadweli Nambari 29 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha Zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 6/8 | 001902 | 900,000 | Lubna Yassir Khalfan | Malipo fedha kwa ajili ya safari kikazi Unguja |
| 2. | 1/9 | 001933 | 831,250 | Ramla Khamis Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula |
| 3. | 4/9 | 001935 | 400,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya kampeni ya VVU na madawa ya kulevya |
| 4. | 7/9 | 001935 | 2,310,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la safari kikazi |
| 5. | 2/10 | 001982 | 2,128,000 | Laki si Pesa | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na vinywaji |
| 6. | 11/10 | 001986 | 200,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 7. | 21/10 | 001994 | 700,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya ada ya masomo |
| 8. | 22/10 | 001994 | 4,000,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwasaidia vikundi vya ushirika |
| 9. | 51/10 | 002005 | 560,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho ya safari kikazi Unguja |
| 10. | 90/10 | 002024 | 10,173,360 | Omar Khamis Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vyoo vya Skuli ya Mjini Wingwi Micheweni. |
| 11. | 98/10 | 002027 | 6,160,839 | Salum Suleiman Hamad (fundi) | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa milango na ukarabati wa Soko la samaki Micheweni. |
| 12. | 103/10 | 002029 | 150,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vespa SMZ 883C |
| 13. | 32/12 | 002091 | 640,000 | Halmashauri ya wilaya ya mcheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la ziada la kujikimu kwa safari kikazi |
| 14. | 48/1 | 002148 | 4,478,490 | Omar Khamis Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa mgahawa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 17. | 33/2 | T/O | 13,547,520 | ZAN IT Sulution Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi Wa CCTV Camera |
| 18. | 21/3 | 001744 | 6,900,000 | Kai Rashid Omar | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kiwanja. |
| 19. | 86/5 | 002309 | 1,100,000 | Halmashauri ya wilaya ya mcheweni | Malipo ya fedha kwa ajili ya kusaidia gharama za uandikishaji wa daftari la wapiga kura |
| **Jumla** | | | **55,179,459** | | |

### 4.7.2 Malipo kwa watoa huduma wasiosajiliwa shilingi 57,316,551

Jumla ya shilingi 57,316,551 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kunyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa orodha ya watoa huduma hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 30: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 11/8, 29/7/2019 | 001899 | 541,500 | Suleiman Said Omar | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya pikipiki |
| 2. | 3/10 | 001982 | 399,000 | Laki si Pesa | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na Vinywaji |
| 3. | 2/10, 26/9/2019 | 001982 | 2,128,000 | Laki si Pesa | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na Vinywaji |
| 4. | 15/10 | 001989 | 529,000 | Ramla Khamis Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Chakula na Vinywaji |
| 5. | 18/10 | 001992 | 247,000 | Laki si Pesa | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Chakula na Vinywaji. |
| 6. | 49/10 | 002004 | 273,125 | Moh`d Issa Moh`d | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Chakula na Vinywaji. |
| 7. | 90/10, 10/10/2019 | 002024 | 10,173,360 | Omar Khamis Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo Skuli ya Mjini Wingwi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | 98/10,<br>30/10/2019 | 002027 | 6,160,839 | Salum Suleiman Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi waMilango na ukarabati wa soko la samaki Micheweni. |
| 9. | 105/10,<br>18/10/2019 | 002030 | 419,215 | How To be Restaurant | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Chakula na Vinywaji. |
| 10. | 47/1,<br>6/1/2020 | 002147 | 5,551,700 | Mohammed Khalfan Adeyum | Ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 11. | 50/1,<br>10/1/2020 | 002150 | 5,575,015 | Hadaa Kombo Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mchanga, mawe na kokoto |
| 12. | 38/3,<br>18/2/2019 | T/O | 3,235,088 | Msabah Masoud Msabah | Malipo ya fedha kwa uwekaji wa Air Condition (installation) |
| 13. | 26/5,<br>16/3/2020 | 002403 | 769,592 | Salum Suleiman Hamad | Malipo kwa ajili ya ukarabati wa mashimo ya maji machafu katika soko la samaki njuguni. |
| 14. | 4/6,<br>1/6/2020 | 002314 | 9,684,466 | Omar Khamis Hamad | Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa ajili ya urekebishaji na umaliziaji wa jengo la nyumba na anadai shilingi 10,500,000 |
| 15. | 14/6,<br>5/6/2020 | 002317 | 1,968,500 | Konde petrol station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel na Petrol. |
| 16. | 36/6,<br>16/6/2020 | 002329 | 9,684,466 | Omar Khamis Hamad | Malipo ya fedha za mwisho kwa ajili ya urekebishaji na umalizikiaji wa jengo la nyumba. |
| **Jumla** | | | **57,339,866** | | |

### 4.7.3 Malipo yaliyofanyika nje ya vifungu vya miradi shilingi 49,458,855

Jumla ya shilingi 49,458,855 zimelipwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakulipwa kwa mujibu vifungu vya miradi husika bila ya kufuata utaratibu wa uhaulishaji.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 75 (7) na kifungu nambari 80 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar nambari 7 ya mwaka 2014. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 31: Malipo yaliyofanyika nje ya vifungu**

| Namba | Mradi uliopangwa | Maelezo ya Mradi uliotekelezwa | Fedha zilizopangwa (Shs.) | Fedha zilizotumika (Shs.) | Tofauti ya Fedha (Shs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukarabati wa barabara za ndani | Ukarabati wa kituo cha Afya Msuka Ungi | 13,000,000 | 11,767,155 | 1,232,845 |
| 2 | Ujenzi wa nyumba ya kupumzikia wageni | Ujenzi wa Mkahawa | 134,000,000 | 37,691,700 | 96,308,300 |
| **Jumla** | | | **147,000,000** | **49,458,855** | **97,541,145** |

### 4.7.4 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari la ghalani shilingi 21,124,230

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya manunuzi ya vifaa mbalimbali venye thamani ya shilingi 21,124,230 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Halmashauri. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havijarikodiwa katika daftari la ghalani.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 32: Vifaa ambavyo havijarikodiwa ghalani**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 34/7 | 001880 | 901,930 | MALINGE ENTR. | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa vya kuandikia kwa ajili ya Ofisi |
| 2. | 1/8 | 01896 | 14,670,600 | Khamis Yussuf Hamad | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Ujenzi |
| 3. | 47/1 | 002147 | 5,551,700 | Mohammed Khalfan Adeyyum | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Ujenzi |
| **Jumla** | | | **21,124,230** | | |

### 4.7.5 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 236,647,141

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shilingi 236,647,141 kwa ajili ya matumizi mbali mbali. Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa hati za malipo husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 33: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 18/7 | 1874 | 1,920,000 | Halmashauri ya wilaya ya micheweni |
| 2 | 33/7 | 1879 | 1,210,260 | Salum Ameir Said |
| 3 | 27/8 | 195 | 240,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 4 | 46/8 | 1914 | 102,917 | Platnam credit ltd |
| 5 | 65/9 | 1964 | 240,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 6 | 10/12 | 1986 | 80,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 7 | 65/10 | 2009 | 916,254 | Sanlam life insurance |
| 8 | 53/11 | 2056 | 560,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 9 | 79/11 | 2070 | 140,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 10 | 47/12 | 2099 | 608,190 | Omar Khamis Hamad |
| 11 | 54/12 | 2107 | 120,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 12 | 58/12 | 2107 | 500,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 13 | 71/12 | T/O | 79,095,320 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 14 | 72/12 | T/0 | 115,331,091 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 15 | 84/1 | T/O | 20,725,000 | Halmashauri ya wilaya ya Micheweni |
| 16 | 26/3 | 2403 | 769,590 | Salum Suleiman Hamad |
| 17 | 4/11 | 2429 | 498,059 | Msabah H. Msabah |
| 18 | 37/4 | 2440 | 463,933 | Omar Khamis Hamad |
| 19 | 5/4 | 2465 | 212,136 | Juma Mjaka Faki |
| 20 | 23/5 | 2474 | 553,398 | Juma Kombo Hija |
| 21 | 36/5 | 2479 | 3,818,000 | Omar Khamis Hamad |
| 22 | 55/5 | 2488 | 3,440,293 | Salum Ameir Said |
| 23 | 56/5 | 2489 | 5,102,700 | Mohd khalfan |
| **Jumla** | | | **236,647,141** | |

### 4.7.6 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya Minara

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakusanya mapato ya Minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo ukaguzi umeshindwa kuona kima halisi cha fedha kilichokusanywa na kampuni hiyo.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Kukusanya mapato kupitia wakala wa ukusanyaji wa mapato ya Minara kunapelekea Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kukosa mapato kwa kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa na Halmashauri bila ya kumtumia Wakala.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kufanya Upembuzi Yakinifu ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za Umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

### 4.7.7 Tofauti katika taarifa za makusanyo ya mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa tofauti katika kumbukumbu za mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Hali ambayo imepelekea ukaguzi kushindwa kujuwa usahihi wa mapato halisi yaliyokusanywa kwa kupitia taarifa za kumbukumbu za mfumo wa mapato, daftari la mapato na taarifa za benki.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuwa makini katika uaandaaji na uwasilishaji wa taarifa za mapato pamoja na kuandaa taarifa ya usuluhishi wa kibenki ili kubaini kasoro zitakazojitokeza katika taarifa hizo.

Mchanganuo wa utofauti wa taarifa za mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 34: Tofauti ya taarifa za mapato**

| Namba | Mwezi | Daftari la uchambuzi wa mapato (Shs.) | Daftari la mapato (Shs.) | Taarifa za Benki (Shs.) | Taarifa za Mfumo (Shs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Julai, 2019 | 13,678,700 | 13,432,100 | 11,820,500 | 6,477,900 |
| 2 | Agost, 2019 | 34,631,500 | 18,232,000 | 18,231,800 | 7,945,400 |
| 3 | Septemba, 2019 | 23,215,600 | 22,838,000 | 22,838,200 | 5,829,600 |
| 4 | Oktoba, 2019 | 12,296,500 | 12,381,471 | 12,382,471 | 10,669,871 |
| 5 | Novemba, 2019 | 17,258,000 | 15,727,200 | 15,727,200 | 9,198,300 |
| 6 | Disemba, 2019 | 17,780,300 | 18,504,300 | 18,504,300 | 15,491,200 |
| 7 | Januari, 2020 | 42,603,300 | 55,090,966 | 54,860,966 | 30,419,600 |
| 8 | Febuari, 2020 | 15,598,800 | 19,457,800 | 19,513,800 | 17,391,300 |
| 9 | Machi, 2020 | 26,275,440 | 27,470,440 | 27,385,440 | 30,457,340 |
| 10 | Aprili, 2020 | 13,760,500 | 15,217,000 | 15,217,000 | 16,256,000 |
| 11 | Mei, 2020 | 26,225,000 | 26,950,000 | 26,925,000 | 27,002,500 |
| 12 | Juni, 2020 | 9,920,000 | 19,081,000 | 19,781,000 | 17,212,000 |
| **Jumla** | | **253,243,640** | **264,382,277** | **263,187,677** | **194,351,011** |

## Maoni ya Ukaguzi

## Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.8 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Mji Chake Chake kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Mji Chake Chake pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza.

**Taarifa ya mapato**

Baraza la Mji Chake Chake lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 600,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni 2020, jumla ya shilingi 523,137,240 zilikusanywa na Baraza sawa na asilimia 97.2 za makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 5,853,203,709 kwa kazi za kawaida na shilingi 165,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 kiasi cha shilingi 6,714,538,954 zimetumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 114.7 ya makadirio na shilingi 160,189,900 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 97.1 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.8.1 Malipo kwa watoa huduma wasiosajiliwa shilingi 6,742,687

Jumla ya shilingi 6,742,687 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Baraza la Mji Chake Chake, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kunyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016. Orodha ya watoa huduma hao ni kama inavyoonekna katika jadweli lifuatalo:-

## Jadweli Nambari 35: Malipo ya watoa huduma ambao hawakusajiliwa

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha iliyotumika (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 120/92, 26/09/2019 | 3871 | 714,000 | Ramla Khamis Juma | Ikiwa ni malipo kwa ajilii ya ununuzi wa chakula, vinywaji na stationary |
| 2 | 121/09, 26/09/2020 | 3871 | 500,000 | Pemba Resturant and Take Away | Ikiwa ni malipo kwa ajilii ya ununuzi wa chakula, vinywaji na stationary |
| 3 | 54/09, 17/9/2020 | 19 | 1,382,250 | Suleiman Massoud Rashid | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya muendelezo wa ujenzi wa Skuli ya Mtimbu |
| 4 | 56/9, 17/9/2019 | 3831 | 87,455 | Hassan Motorcycle Spare Part | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mpira wa bero, engine oil na gear oil ya Passola. |
| 5 | 58/9, 17/9/2019 | 3835 | 241,080 | Mbarouk Salum Ali | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ujenzi |
| 6 | 59/9, 17/9/2019 | 3835 | 419,440 | Mbarouk Salum Ali | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 7 | 30/12, 5/12/2019 | 4068 | 290,000 | Hasina Catering and Take Away Service | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya chai na viburudisho |
| 8 | 23/7, 17/7/2019 | 3685 | 484806 | Mums Food & Refreshment | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa chai, chakula, na vinywaji |
| 9 | 26/7, 18/7/2019 | 3688 | 1,711,080 | Ramla Khamis Juma | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya chakula na vinywaji. |
| 10 | 32/8, 5/8/2019 | 3746 | 912,576 | Uchida Services And Maintanance | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa kipozea joto (AC) na Switch socket |
| **Jumla** | | | **6,742,687** | | |

### 4.8.2 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 22,061,970

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Chake Chake limefanya malipo ya shilingi 22,061,970 kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa hati za malipo husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 36: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 28/9 | 3817 | 1,140,720 | Hasina Catering & Take away |
| 2 | 127/9 | 3873 | 6,490,000 | Baraza la Mji Chake |
| 3 | 128/9 | 3875 | 6,490,000 | Baraza la Mji Chake |
| 4 | 69/10 | 3913 | 5,941,250 | Mbarka M. Omar |
| 5 | 70/10 | 3914 | 2,000,000 | Shirika la Umeme |
| **Jumla** | | | **22,061,970** | |

### 4.8.3 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 32,388,860

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Chake Chake limefanya malipo ya shilingi 32,388,860 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 37: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha Ziliyolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 93/7 | 003725 | 820,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za safari kikazi Dar es Salaam kufuatilia vifaa vya incinerator. |
| 2. | 2/10 | 003883 | 1,212,800 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za uji na umeme kwa skuli za maandalizi za Wilaya ya Chake Chake. |
| 3. | 1/3 | 004241 | 1,570,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za uji na umeme kwa skuli za maandalizi za Wilaya ya Chake Chake. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. | 29/11<br>5/11/2019 | 003987 | 1,140,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya kutoa elimu ya Afya na ukaguzi wa usafi kwa ajili ya kulipwa Wafanyakazi wa Idara ya Afya. |
| 5. | 30/11<br>04/11/2019 | 003987 | 520,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za safari kimatibabu Unguja. |
| 6. | 71/4 | 004331 | 1,200,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara ya vibarua wa muda wa BLM Chake kwa mwezi wa Dec 2019. |
| 7. | 13/11<br>03/11/2019 | 003978 | 545,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za safari kikazi Unguja. |
| 8. | 138/11<br>29/11/2019 | 004048 | 700,000 | Ibrahim Salim Rashid | Malipo ya fedha za safari kikazi Unguja. |
| 9. | 127/11<br>28/11/2019 | 004049 | 500,000 | Zanzibar Telecom Co.LTD | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vocha. |
| 10. | 59/10<br>12/10/2019 | 003911 | 614,400 | Misufini Stationery Centre | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa hewa ya liquid nitrogen na vifaa vya kuendeshea mafunzo. |
| 11. | 62/10<br>16/10/2019 | 003912 | 1,855,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha ya safari kikazi Tanga. |
| 12. | 63/10<br>16/10/2019 | 003912 | 860,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha ya safari kikazi Tanga. |
| 13. | 34/11<br>06/11/2019 | 003987 | 590,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha ya safari kikazi Unguja. |
| 14. | 66/08<br>16/08/2019 | 003769 | 1,680,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha ya safari kikazi Unguja. |
| 15. | 104/8<br>24/08/2019 | 003794 | 1,200,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara ya vibarua wa muda wa BLM Chake. |
| 17. | 87/08<br>20/08/2019 | 003784 | 770,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za posho la safari ya Unguja. |
| 18. | 106/8<br>22/08/2019 | 003794 | 1,000,000 | Baraza la Mji Chake Chake | Malipo ya posho la Chakula katika mafunzo ya utunzaji mazingira. |
| 19. | 105/8<br>24/08/2019 | 003794 | 4,750,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za posho kwa madiwani |
| 20. | 40/11<br>07/11/2019 | 003992 | 2,140,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya posho kwa kikao cha madiwani . |
| 21. | 47/11<br>11/11/2019 | 003998 | 1,022,865 | Ramla Khamis Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula na vinywaji kwa vikao viwili "2" tofauti. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 22. | 15/11<br>27/10/2019 | 003978 | 1,681,400 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya uji, maji na umeme kwa skuli za maandalizi. |
| 23. | 123/10<br>24/10/2019 | 003950 | 1,200,000 | Baraza la Mji Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara ya vibarua wa muda wa BLM Chake kwa mwezi wa Oktoba 2019. |
| 24. | 130/10<br>25/102019 | 003951 | 2,440,000 | Ahmed Rashid Hamad | Malipo ya fedha za Michoro ya Ramani. |
| 25. | 102/9<br>2/9/2019 | 003870 | 1,200,000 | Baraza La Mji Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara ya vibarua wa muda wa BLM Chake**.** |
| 26. | 1/3 | 004241 | 1,570,000 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za uji na umeme kwa skuli za maandalizi za Wilaya ya Chake Chake**.** |
| 27. | 2/10 | 003883 | 1,212,800 | BLM Chake Chake | Malipo ya fedha za uji na umeme kwa skuli za maandalizi za Wilaya ya Chake Chake |
| 28. | 27/9<br>9/9/2019 | 003816 | 1,497,195 | Moh'd Aboud Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 29. | 140/9<br>30/9/2019 | 003879 | 500,000 | Baraza la Mji Chake Chake | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula na vinywaji. |
| **Jumla** | | | **32,388,860** | | |

### 4.8.4 Malipo yaliyofanyika nje ya mkataba shilingi 14,571,876

Baraza la Mji Chake Chake limeingia mkataba wa usafi wa Mji kwa kipindi cha miezi mitatu na kampuni ya usafi ya Task Force for Environment.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza limeipatia Kampuni hiyo gari la kubebea Taka, Dereva, vifaa vya usafishaji pamoja na mafuta ya petroli lita 6,558 kinyume na mkataba, ambapo jumla ya shilingi 14,571,876 zimelipwa kwa Kampuni kwa ajili ya huduma ya usafi wa Mji katika kipindi cha mwaka 2019/2020.

Kufanya malipo nje ya Mkataba kunaweza kupelekea upotevu wa fedha na rasilimali za Umma pamoja na kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### 4.8.5 Kukosekana kwa thamani ya ujenzi wa vyoo vya Skuli ya Maandalizi Mtimbu Pujini shilingi 10,000,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 10,000,000 zimelipwa kwa msambazaji Omar Hamad Kombo kupitia hati ya malipo nambari 12/8 ya tarehe 1/8/2019 kwa hundi nambari 003731 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ikiwemo Mawe Trips 12, Matufali Pcs 3500, Mchanga Trips 6, Kokoto Trips 4, Saruji Pkts 210, Nondo mm 12 Pcs 12, Nondo mm 10 Pcs 55, Nondo mm 6 Pcs 20, Mbao 2x2, Pcs 130, Mbao 1x8 Pcs 120, Binding Wire Roli 5.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba thamani ya vifaa hivyo hailingani na ujenzi wa vyoo hivyo pia ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

### 4.8.6 Mapato ambayo hayakuwasilishwa benki shilingi 48,085,000

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa makusanyo yenye jumla ya shilingi 48,085,000 ambayo yameonekana kukusanywa kupitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato (Revenue Collection System) wa Baraza la Mji la Chake Chake. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mapato hayo hayawasilishwi benki kupitia hesabu ya mapato ya Baraza. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha za mapato pamoja na kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 38: Mapato ambayo hayakuwasilishwa benki**

| Namba | Vyanzo vya mapato | Fedha za mapato kupitia Mfumo (Shs.) | Fedha za mapato kupitia Hesabu ya Benki (Shs.) | Tofauti ya Fedha ambazo hazikuwasilishwa Benki (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada za Usafi | 36,162,000 | 34,608,000 | 1,554,000 |
| 2 | Ushuru wa usafirishaji wa Maliasili Kware | 16,930,000 | 15,420,000 | 1,510,000 |
| 3 | Leseni za Biashara | 151,697,000 | 122,852,000 | 28,845,000 |
| 4 | Ada ya Maegesho | 44,550,500 | 44,283,000 | 267,500 |
| 5 | Ushuru wa bidhaa na huduma kwa kila siku | 15,909,000 | - | 15,909,000 |
| **Jumla** | | **265,248,500** | **217,163,000** | **48,085,500** |

### 4.8.7 Kushindwa kwa Baraza kukusanya ada ya usafi shilingi 33,864,000

Baraza la Mji Chake Chake lina wajibu wa kusimamia na kukusanya mapato kupitia ada ya usafi katika maduka 634 kati ya maduka 1,252 yaliyopo katika Wilaya ya Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo kila duka linapaswa kulipia shilingi 9,000 kwa mwezi.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza limeshindwa kukusanya jumla ya shilingi 33,864,000 zitokanazo na ada ya usafi ambapo ni kuikosesha serikali mapato na kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa.

Orodha ya maduka yanayopaswa kulipa ada ya usafi pamoja na taarifa za makusnyo hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 39: Mapato yatokanayo na ada ya usafi**

| Namba | Anuani | Idadi ya maduka | Mapato yanayopaswa kukusanywa kwa mwezi (Shs.) | Mapato yanayopaswa kukusanywa kwa mwaka (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Miembeni | 198 | 1,782,000 | 21,384,000 |
| 2 | Sokoni | 63 | 567,000 | 6,804,000 |
| 3 | Mkungu Malofa | 112 | 1,008,000 | 12,096,000 |
| 4 | Misufini | 112 | 1,008,000 | 12,096,000 |
| 5 | Madungu | 47 | 423,000 | 5,076,000 |
| 6 | Machomane | 102 | 918,000 | 11,016,000 |
| **Jumla** | | **634** | **5,706,000** | **68,472,000** |
| Mapato ambayo yamekusanywa | | | | **34,608,000** |
| Tofauti ya mapato ambayo hayakukusanywa | | | | **33,864,000** |

### 4.8.8 Kutokuonyeshwa kwa mapato katika taarifa za hesabu shilingi 21,355,000

Jumla ya shilingi 21,355,000 ni fedha za mapato zilizokusanywa na Baraza la Mji la Chake Chake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kwamba fedha za makusanyo hayo hazikuripotiwa na kuonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka husika. Kutokuingizwa na kuonyeshwa mapato hayo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa ya mapato kutokuonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Yenye Shaka**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Mji Chake Chake limepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.9 BARAZA LA MJI MKOANI

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Mji Mkoani kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Mji Mkoani pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza.

**Taarifa ya mapato**

Baraza la Mji la Mkoani lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 340,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 341,944,368 zilikusanywa na Baraza ikiwa sawa na asilimia 100.57 ya makadirio.

**Taarifa ya matumizi**

Baraza la Mji la Mkoani lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,542,841,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 386,137,890 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 1,333,084,945 zimetumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 86.4 ya makadirio na shilingi 200,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 52 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.9.1 Malipo kwa watoa huduma waliokuwa hawakusajiliwa shilingi 11,608,453

Jumla ya shilingi 11,608,453 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Baraza la Mji la Mkoani. Ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kunyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Orodha ya watoa huduma hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 40 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Jumla ya fedha (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 50/3, 10/3/2020 | 3942 | 1,140,720 | Emerald Bay House | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula |
| 2 | 30/7, 9/7/2019 | T.O | 1,017,142 | Suleiman Seif Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| 3 | 36/07, 10/7/2019 | 3498 | 530,434 | Suleiman Seif Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa vifaa vya maji |
| 4 | 24/07, 5/7/2019 | 3489 | 1,239,800 | Suleiman Seif Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme. |
| 5 | 45/10, 17/10/2019 | 3695 | 500,000 | Khamis Othman Hassan | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| 6 | 4/2, 3/2/2020 | 3858 | 1,264,298 | Juma Faki Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 7 | 6/2, 3/2/2020 | 3862 | 1,581,323 | Suleiman Seif Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi |
| 8 | 13/02, 4/2/2020 | 3866 | 3,003,896 | Hamad Said Bakar | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 9 | 1/1, 1/11/2019 | 3722 | 1,330,840 | Ahmed Rajab (Emerald Bay) | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula |
| **Jumla** | | | **11,608,453** | | |

### 4.9.2 Vifaa ambavyo havikurikodiwa kwenye daftari la ghalani shilingi 23,634,109

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji la Mkoani limefanya matumizi ya jumla ya shilingi 23,634,109 kwa ajili ya manunuzi ya mafuta na vifaa mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havikurikodiwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 41: Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 9/8, 1/8/2019 | 3548 | 3,759,623 | Nourbhai Auto Services |
| 2 | 15/1, 2/1/2020 | 3802 | 1,787,128 | Nourbhai Auto Services |
| 3 | 14/01, 3/1/2020 | 3801 | 2,851,000 | Suleiman Seif Rashid |
| 4 | 103/9 | T.O | 1,000,000 | Bakar Petrol Station |
| 5 | 112/8 | T.T | 2,221,000 | Bakar Petrol Station |
| 6 | 83/12 | T.O | 2,270,000 | Bakar Petrol Station |
| 7 | 71/01, 29/01/2020 | 3848 | 3,505,810 | Mtambile Petrol Station |
| 8 | 85/01, 2/1/2020 | T.O | 3,577,868 | Pemba General Supply |
| 9 | 78/03 | 3962 | 2,661,680 | Vista Auto Parts |
| **Jumla** | | | **23,634,109** | |

### 4.9.3 Ulipaji wa masurufu kinyume na utaratibu shilingi 24,410,000

Jumla ya shilingi 24,410,000 zimelipwa kwa njia ya masurufu kwa ajili ya uendeshaji wa chanjo ya rubela na surua katika Wilaya ya Mkoani. Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya masurufu hayo yamelipwa kupitia Mkaguzi wa Ndani wa Baraza kinyume na taratibu za malipo, ambapo Mkaguzi wa Ndani hakupaswa kupewa fedha hizo kwa ajili ya malipo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maadili ya ukaguzi, aidha ni kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika matumizi ya masurufu.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 42: Masurufu yaliyolipwa kinyume na utaratibu**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 84/9 | 003646 | 6,550,000 | Mkaguzi wa Ndani | Malipo ya masurufu kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa kampeni ya Rubela na Surua |
| 2. | 94/9 | 003660 | 17,860,000 | Mkaguzi wa Ndani | Malipo ya masurufu kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa kampeni ya Rubela na Surua |
| **Jumla** | | | **24,410,000** | | |

### 4.9.4 Dosari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa miradi mbali mbali iliyotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika utekelezaji wa miradi hiyo imebainika kuwepo kwa dosari zilizosababishwa na kutokufuatwa kwa taratibu za kisheria za utekelezaji wa miradi husika.

Dosari hizo zimebainika wakati wa kuhakiki Mpango kazi wa Baraza, Mpango wa ununuzi, taratibu za ununuzi, mikataba ya miradi, na taratibu za malipo. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli nambari 43: Miradi iliyotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani**

| Namba | Aina ya mradi | Hatua ya utekelezaji wa Mradi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Chanzo cha Fedha za Mradi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa vyoo vya jamii Mwambe | Mradi haujakamilika | 16,279,000 | Mchango wa Serikali |
| 2 | Ukarabati wa skuli ya maandalizi Mtuhaliwa | Mradi umekamilika | Taarifa za fedha hazikupatikana kwa ukaguzi | Wahisani wa maendeleo |
| 3 | Ukarabati wa skuli ya maandalizi Mtuhaliwa | Mradi umekamilika | 35,000,000 | Mchango wa Serikali |
| 4 | Ukarabati wa barabara chokaani | Mradi upo katika hatua ya Kifusi | 35,000,000 | Wahisani wa maendeleo |
| 5 | Kituo cha mama na mtoto Tironi | Mradi upo katika hatua ya Linta | 23,759,000 | Wahisani wa maendeleo |

**Dosari zilizojitokeza katika utekelezaji wa Miradi hiyo ni kama zifuatazo:-**

i. Kutokuwasilisha kwa Mpango wa Manunuzi wa mwaka kama ilivyoelezwa katika Kifungu nambari 42 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

ii. Wajumbe walioteuliwa katika Kamati ya Tathmini ya miradi iliyotekelezwa hawakukidhi vigenzo kutokana na kutokuwa na barua za uteuzi, hati za kiapo cha maadili na pia kukosa uzowefu unaohitajika katika utekelezaji wa miradi hiyo jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 32 cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

iii. Mikataba yote haijaeka muda wa uangalizi wa utekelezaji wa miradi (defect liability period).

iv. Manunuzi katika miradi yamefanywa kupitia njia ya kugawanya manunuziili kukwepa ushindani jambo ambalo linakwenda kinyume na Kifungu nambari 42 (2) (c) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

## 88.0 Mapungufu katika ujenzi wa ofisi ndogo ya Baraza shilingi 199,718,400

Barara la Mji Mkoani limeingia mkataba wa ujenzi wa Ofisi ndogo na Kampuni ya Zenji Building Construction Ltd kwa thamani ya shilingi 199,718,400 ili kuondoa tatizo la ufinyu wa eneo la kufanyia kazi.

Kupitia ujenzi huo ukaguzi umebaini dosari mbali mbali kama zifuatazo:-

- Utaratibu usioridhisha wa kumpata mkandarasi wa ujenzi ikiwemo kutokuwepo kwa vikao vya tathmini ya ujenzi, vikao vya kufanya maamuzi ya kuanza kwa ujenzi, vikao vya kuitisha tenda, vikao vya kuzipitia na kumpata mkandarasi aliyekidhi vigezo.
- Kutokuwepo kwa mshauri elekezi kwa ajili ya kulishauri Baraza juu ya utaratibu wa ujenzi.
- Kutokuwepo kwa tarehe ya kuanza na kumalizika kwa ujenzi ndani ya mkataba.
- Pamoja na kutumia jumla ya shilingi 125,052,000 kati ya shilingi 169,252,880 ikiwa sawa asilimia 74 ya fedha zote za mkataba, ukaguzi umebaini kutokukamilika kwa vipengele vifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 44: Kazi za ujenzi ambazo hazijaanza kutekelezwa**

| Namba | Kazi ambazo hazijafanywa | Jumla ya fedha zilizokadiriwa (Shs.) |
|---|---|---|
| 1 | Kazi za umaliziaji (Finishing works) | 43,090,000 |
| 2 | Milango na Madirisha (Doors and Windows) | 25,680,000 |
| 3 | Mifumo ya maji safi na maji taka (Plumbing Works) | 4,382,000 |
| 4 | Vipengele vyenginevyo ikiwemo kuweka umeme, Uwekaji wa tanki na shimo | 12,000,000 |
| **Jumla** | | **85,152,000** |

### Maoni ya Ukaguzi

### Hati yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Mji Mkoanikwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 hazionyeshi sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Mji Mkoani limepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

## 4.10 BARAZA LA MJI WETE

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Mji Wete kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, umefanywa kwa kufuata sheria , kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Mji Wete pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri.

### Taarifa ya mapato

Baraza la Mji Wete lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 325,000,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 359,468,990 zilikusanywa na Baraza la Mji Wete ikiwa sawa na asilimia 110.60 ya makadirio.

**Taarifa za matumizi**

Baraza la Mji Wete lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 6,348,959,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 125,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa mwaka 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 6,798,347,585 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 107.08 ya makadirio na shilingi 57,000,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 45.60 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

### 4.10.1 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 72,081,914

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Mjini limefanya malipo ya shilingi 33,674,900 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 45: Malipo yaliyokosa vielelezo**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 77/7 | T.T | 1,843,000 | Rassco Co. Ltd | Malipo ya fedha kwa kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Julai, 2019 |
| 2. | 78/7 | T.T | 1,843,000 | Peso | Malipo ya fedha kwa kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Julai, 2019 |
| 3. | 1/8 | 669971 | 1,568,490 | Seif Haji Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Fusi. |
| 4. | 26/8 | 669971 | 950,000 | Moh`d Khalfan Adeyum | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa bati za msaada kwa mfanyakazi aliyefikwa na maafa |
| 5. | 26/8 | 669975 | 200,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa aijli ya matumizi mbali mbali ya ofisi |
| 6. | 64/8 | 669976 | 3,405,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho kwa mafunzo ya kamati za kilimo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. | 75/8 | 669978 | 11,692,380 | Masoud Abrahman Masoud | Malipo ya fedha kwa ajili ya kumlipa Fundi kwa ujenzi wa ofisi |
| 8. | 89/8 | 669985 | 545,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwaajili ya nauli na posho safari kikazi |
| 9. | 83/8 | 669985 | 270,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa godoro na mchele kuwafariji wananchi waliopatwa na maafa |
| 10. | 98/8 | 669986 | 300,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwaajili ya chakula na viburudishaji |
| 11. | 122/8 | 669991 | 360,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwaajili ya posho na viburudishaji kwa wajumbe wa Kamati ya mipango |
| 12. | 137/8 | 669991 | 541,842 | Khashiya Vanue and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji kwa kikao cha walimu na Mkurugenzi |
| 13. | 127/8 | 669993 | 408,758 | Ali Salum Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya uchoraji wa mabango ya Skuli. |
| 14. | 136/8 | 669997 | 1,040,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya kulipa posho kwa wafanyakazi waliohudhuria katika tathmini ya vituo vya Afya. |
| 15. | 36/9 | | 1,843,000 | PESO | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikun-di cha usafishaji taka kwa mwezi wa August-2019 |
| 16. | 37/9 | | 1,843,000 | RASSCO CO. Ltd | Ikiwa nimalipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikun-di cha usafishaji taka |
| 17. | 26/8 | 670162 | 590,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwaajili ya nauli na posho safari kikazi |
| 18. | 31/10 | 670063 | 1,620,000 | Baraza la Mji wete | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa bendera 27 kwa skuli za msingi za wilaya ya wete. |
| 19. | 34/10 | 670063 | 530,000 | Baraza la Mji Wete | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitu mbali mbali. |
| 20. | 81/10 | 670078 | 1000,000 | Rashid Ali Makame | Malipo kwa ajili ya kutayarisha Shamba la kilimo cha pilipilli ili kuwawezesha Baraza la vijana kiuchumi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 21. | 70/10 | 670072 | 2,151,208 | MALINGE ENTEPRISES | Malipo ya fedha kwa ajil ya ununuzi wa stationary. |
| 22. | 17/2 | 670218 | 3,322,034 | Massoud Abrahman Massoud | Malipo ya fedha kwa ajil ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 23. | 24/2 | 670219 | 1,455,728 | Chasasa Services Stationery | Malipo ya ununuzi wa ma-futa kwa matumizi ya ofisi |
| 24. | 24/2 | 670223 | 750,000 | Rashid Salum Abdulaziz | Malipo ya fedha za awamu ya mwisho ya kumalizia ujenzi wa skuli ya maan-dalizi Jadida |
| 25. | 38/2 | 670230 | 1,699,029 | Khashya Vanue And Refreshment | Malipo ya fedha za vibu-rudisho kwa ajili ya kikao cha madiwani. |
| 26. | 40/2 | T.T | 1,843,000 | Rassco Co. Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Januari, 2020. |
| 27. | 41/2 | T.T | 1,843,000 | Peso | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Januari, 2020. |
| 28. | 42/2 | T.T | 1,098,000 | Stone Town Traders | Malipo ya fedha kwa ajili ya uchapishaji wa diary kwa matumizi ya ofisi |
| 29. | 43/2 | T.T | 1,843,000 | Pemba Strengtheng Organization | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Januari, 2020. |
| 30. | 7/3 | 670235 | 1,410,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kujikimu kwa watendaji walioshiriki vikao vya mapitio ya bango kitita |
| 31. | 23/3 | 670235 | 1,260,000 | Baraza la Mji Wete | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya wahudumu waliotoa huduma ya mkoba (OUTRICH) kwa mwezi wa December 2019 |
| 32. | 8/3 | 670235 | 590,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la siku mbili pamoja na nauli ya safari kikazi Unguja |
| 33. | 3/3 | 670235 | 555,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli la safari kikazi Unguja |
| 34. | 22/5 | 670315 | 590,000 | Baraza la mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la safari kikazi Unguja |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 35. | 32/5 | 670316 | 3,597,087 | Salim Khamis Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kifusi trips 13 kwa matengenezo ya barabara |
| 36. | 38/5 | 670317 | 210,000 | Baraza la mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli la safari kikazi Unguja |
| 37. | 46/5 | 670318 | 890,000 | Baraza la mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la safari kikazi Unguja |
| 38. | 49/5 | 670320 | 2,029,126 | Salim Khamis Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kifusi trips 13 kwa matengenezo ya barabara |
| 39. | 52/5 | 670323 | 1,208,252 | Salim Khamis Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kifusi trip 9 kwa matengenezo ya barabara |
| 40. | 8/5 | 6703O7 | 550,000 | Baraza la mji Wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli ya safari kikazi Unguja. |
| 41. | 35/6 | T.T | 1,260,000 | Bright Security company | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Mei, 2020. |
| 42. | 36/6 | T.T | 1,844,660 | Rassco Co. LTD | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Mei, 2020. |
| 43. | 37/6 | T.T | 1,844,660 | Pemba Strengthening Organization | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka kwa mwezi wa Mei, 2020. |
| 44. | 29/6 | 670332 | 1270,000 | Baraza la miji wete | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli ya safari kikazi Unguja. |
| 45. | 10/6 | T.T | 1,844,660 | PESO | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka katika maeno ya mji wa wete. |
| 46. | 2/6 | 670328 | 2,730,000 | Baraza la Mji Wete | Malipo ya fedha kwajili ya safari kikazi Unguja |
| **Jumla** | | | **72,081,914** | | |

### 4.10.2 Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa shilingi 14,900,079

Jumla ya shilingi 14,900,079 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Baraza la Mji Wete, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kunyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016. Orodha ya watoa huduma hao ni kama inavyoonekna katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli nambari 46: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha zilizolipwa (Shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 138/8 30/8/2019 | 669999 | 903,070 | Khashiya Venue and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji. |
| 2. | 137/8 30/8/2019 | 669998 | 541,842 | Khashiya Venue and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji. |
| 3. | 126/8 29/8/2019 | 669992 | 427,770 | Khashiya Venue and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji |
| 4. | 13/5 8/5/2020 | 670310 | 1,902,913 | Omar Breik Omar | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi |
| 5. | 98/9 18/9/2019 | 670036 | 2,842,294 | Moh'd Khalfan Adeyoum | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 6. | 116/9 26/9/2019 | 670043 | 506,825 | Khamid Shamis Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya kumlipa fundi |
| 7. | 12/7 12/7/2019 | 669943 | 427,770 | Kashiya venue & refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji |
| 8. | 99/9 20/9/2019 | 670037 | 1,336,175 | Salmin Juma Khamis | Malipo ya fedha kwa ajii ya kazi ya ufundi kwa awamu ya mwisho |
| 9. | 35/6 | T.T | 1,260,000 | Bright Security Company | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 20. | 36/9<br>9/9/2019 | | 1,843,000 | PESO | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka |
| 11. | 37/9<br>9/9/2019 | | 1,843,000 | RASSCO.Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa kikundi cha usafishaji taka |
| 12. | 77/8<br>09/8/2019 | 669975 | 665,420 | Khashiya Venue and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji. |
| 13. | 36/8<br>5/8/2019 | 669975 | 400,000 | Baraza la Mji (Khashiya Venue and Refreshment) | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji. |
| **Jumla** | | | **14,900,079** | | |

### 4.10.3 Kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa shilingi 68,000,000

Baraza la Mji Wete lilipanga kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo yenye jumla ya shilingi 68,000,000. Ukaguzi umebaini kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa ingawa Baraza lilikusanya jumla ya mapato ya shilingi 359,468,990 sawa na asilimia 110.6 ya makadirio kukiwa na ongezeko la shilingi 34,468,990 ambayo ni sawa na asilimia 10.6 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nambari 7 ya mwaka 2014 pamoja na sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli nambari 47: Miradi ambayo haikutekelezwa**

| Namba | Mradi uliopangwa kutekelezwa | Jumla ya fedha zilizokadiriwa (Shs.) |
|---|---|---|
| 1 | Uwezekaji wa vyumba vitano "5" vya Skuli ya Maziwani | 30,000,000 |
| 2 | Ukarabati wa Skuli ya Ukunjwi Msingi | 14,000,000 |
| 3 | Ukarabati wa Skuli ya Kiungoni Msingi | 14,000,000 |
| 4 | Ujenzi wa Slab maeneo ya Mji wa Wete | 10,000,000 |
| **Jumla** | | **68,000,000** |

### 4.10.4 Kutokuonyeshwa kwa mapato katika taarifa za hesabu shilingi 34,140,000

Jumla ya shilingi 34,140,000 ikiwa ni fedha za mapato zilizokusanywa na Baraza la Mji la Wete kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kwamba fedha hizo za makusanyo yatokanayo na utoaji wa vibali vya ujenzi hazikuripotiwa na kuonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

Kutokuingizwa na kuonyeshwa mapato hayo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa ya mapato kutokuonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 48 : Stakabadhi za mapato ambazo hazikuoneshwa**

| Namba | Mtiririko wa nambari za Stakabadhi | Jumla ya fedha zilizokusanywa (Shs.) |
|---|---|---|
| 1 | 399401 – 399450 | 3,040,000 |
| 2 | 399451 – 399500 | 3,700,000 |
| 3 | 1173101 – 1173150 | 3,060,000 |
| 4 | 1176101 – 1176150 | 4,060,000 |
| 5 | 1176451 – 1176500 | 2,750,000 |
| 6 | 32451 – 32500 | 2,820,000 |
| 7 | 34101 – 34150 | 2,380,000 |
| 8 | 33801 – 33850 | 2,560,000 |
| 9 | 134951 – 135000 | 3,080,000 |
| 10 | 408201 – 408250 | 460,000 |
| 11 | 219401 – 219450 | 3,180,000 |
| 12 | 144051 – 144100 | 3,050,000 |
| **Jumla** | | **34,140,000** |

**Maoni ya Ukaguzi**

**Hati Inayoridhisha yenye Aya ya Msisitizo**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Baraza la Mji la Wete kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Baraza la Mji la Wete limepata hati inayoridhisha yenye aya ya msisitizo kutokana na hoja zilizoainishwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

# SURA YA TANO

## 5.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA YA HOJA ZA UKAGUZI ZILIZOBAINIKA

Sura hii inaonesha mapendekezo ya jumla juu ya hoja za ukaguzi zilizobainika katika ukaguzi wa hesabu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali ambazo zilipelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi, dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

1) Kutokuwepo kwa mfumo imara wa udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
2) Kutokufuatwa kwa sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya.
3) Kutokuwepo na mfumo wa utunzaji wa mali za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
4) Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa udhibiti wa ukusanyaji wa mapato.
5) Kuwepo kwa dosari katika utayarishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

Kufuatia kubainika kwa dosari hizo, ukaguzi unapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe kwa madhumuni ya kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufuata sheria na kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

## 5.1 Kuimarishwa kwa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa baadhi ya Halmashauri na Manispaa kutokuwa na Kamati za Ukaguzi wa Ndani au kutokufanyakazi kwa kamati hizo. Kutokufanyakazi kwa Kamati za Ukaguzi wa Ndani kunaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kuchukuliwa hatua za awali pale zinapojitokeza.

Aidha ukaguzi umebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani (Internal Audit Units) katika Halmashauri na Manispaa zilizokaguliwa hazikuwasilisha taarifa za ukaguzi wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa katika Kifungu namba 117 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri kuimarishwa kwa mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kuanzisha Kamati za Ukaguzi na kushajihisha zifanye kazi zake kwa mujibu wa sheria, aidha ukaguzi unashauri vitengo vya ukaguzi wa ndani vya Halmashauri pamoja na Manispaa kuandaa ripoti za ukaguzi wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu namba 117(6).

## 5.2 Kufuatwa kwa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

Ukaguzi ulibaini kutokufuatwa kikamilifu kwa sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya, dosari zilizobainika ni kukiukwa kwa taratibu za manunuzi kama zilivyoelekezwa katika sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma pamoja na kufanyika kwa taratibu za manunuzi ambazo hazikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni za Halmashauri husika.

Ukaguzi unapendekeza kufuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na kuziimarisha Bodi za Zabuni zifanye kazi zake kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

## 5.3 Kuwepo kwa Mfumo mzuri wa Udhibiti wa Mali za Kudumu

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mfumo wa udhibiti wa mali za kudumu kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya pamoja na Manispaa hali ambayo inaweza kupelekea upotevu au uharibifu wa mali hizo. Ukaguzi unapendekeza kuanzishwa kwa Mfumo wa Udhibiti wa Mali za Kudumu kwa kuziingiza katika kumbukumbu za mali za Halmashauri na Manispaa hizo ili kuweka udhibiti na utunzaji wa mali hizo.

## 5.4 Kuwepo kwa mfumo mzuri wa udhibiti wa ukusanyaji wa mapato

Ukaguzi ulibaini dosari katika mfumo wa udhibiti wa ukusanyaji wa mapato kwa baadhi ya Halmashauri na Manispaa, kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa udhibiti wa ukusanyaji wa mapato kunaweza kupelekea uvujaji wa mapato husika na kupelekea malengo yaliyokusudiwa kutofikiwa.

Ukaguzi unapendekeza kuimarishwa kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha mapato yote yanayokusanywa yanaripotiwa katika vitabu vya mapato na kuwasilishwa benki kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

Aidha ukaguzi unapendekeza kuwepo kwa mfumo mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu za stakabadhi za mapato kwa kuhakikisha kumbukumbu hizo zinatunzwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

## 5.5 Kuwepo kwa Mfumo wa utayarishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka

Ukaguzi umebaini dosari katika utayarishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya, dosari hizo ni kutokufuatwa kwa viwango vya utayarishaji wa hesabu na kutokuwepo na Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kuwepo kwa dosari katika utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea baadhi ya taarifa za hesabu hizo kutoonyesha sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unapendekeza kuwepo kwa mfumo wa utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na kuanzishwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mapato na Matumizi utakaounganishwa kwa Halmashauri na Manispaa za Wilaya.

# VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO NAMBARI 1: Vitabuvyastakabadhiambavyohavikupatikana kwa ukaguzi - Baraza la Manispaa Manispaa ya Mjini Zanzibar.**

| Namba | Tarehe | Mtiririko wa nambari za stakabadhi | Aliyepewa |
|---|---|---|---|
| 1 | 16/12/19 | 53051-53100 | Khadija Kessi |
| 2 | 20/12/19 | 53551-53600 | Asha Juma |
| 3 | 20/12/19 | 53601-53650 | Tatu Ahmada |
| 4 | 23/12/19 | 53751-53800 | Masemo Ahmada |
| 5 | 23/12/19 | 53801-53850 | Amina Abdalla |
| 6 | 24/12/19 | 53951-54000 | Asiya Omari |
| 7 | 24/1/19 | 57351-57400 | Omari Amani |
| 8 | 3/6/20 | 63451-63500 | Asya Omar Makame |
| 9 | 16/5/20 | 63601-63650 | Masemo Ahmada |
| 10 | 19/5/20 | 63751-63800 | Zamzam Amour |
| 11 | 27/5/20 | 63951-64000 | Asha Said |
| 12 | 21/5/20 | 63851-63900 | Asha J Khamis |
| 13 | 11/6/20 | 64851-64900 | Asha Said |
| 14 | 12/6/20 | 65551-65600 | Tatu Ahmada |
| 15 | 16/6/20 | 65601-65650 | Zulfa A Khatib |
| 16 | 17/6/20 | 65701-65750 | Miski Bakar |
| 17 | 19/6/20 | 65851-65900 | Asya Omar Makame |
| 18 | 24/6/20 | 66001-66050 | Asha Said |
| 19 | 1/7/19 | 15351-15400 | Mtumwa Bande |
| 20 | 2/7/19 | 15301-15351 | Zamzam Amour |
| 21 | 2/7/19 | 15461-15450 | Tatu Salum Issa |
| 22 | 2/7/2019 | 15451-15500 | Tatu Ahmada |
| 23 | 2/7/19 | 15501-15550 | Tatu Ahmada |
| 24 | 2/7/19 | 15551-15600 | Bimkubwa Khatib |
| 25 | 3/7/19 | 15601-15650 | Maulid /A/ Maulid |
| 26 | 3/7/19 | 15651-15700 | Mwanamanga Juma |
| 27 | 3/7/19 | 15701-15750 | Mwanamanga Juma |
| 28 | 3/7/19 | 15751-15800 | Zulfa Abdi |
| 29 | 3/7/19 | 15801-15850 | Asha Juma Khamis |
| 30 | 3/7/19 | 15851-15900 | Masemo Ahmada |
| 31 | 3/7/19 | 15901-15930 | Mtumwa Bande |
| 32 | 4/7/19 | 15951-16000 | Ali Omar |
| 33 | 5/7/19 | 16051-16100 | Wahida Omar |
| 34 | 5/7/19 | 16101-16150 | Zulfa Abdi |
| 35 | 5/7/19 | 16151-16200 | Tatu Ahmada |
| 36 | 5/7/19 | 16201-16250 | Asha Hussein |
| 37 | 7/7/19 | 16251-16300 | Khadija Kessi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 38 | 9/7/19 | 16401-16450 | Zulfa Abdi |
| 39 | 9/7/19 | 16451-16500 | Masemo Ahmada |
| 40 | 9/7/19 | 16501-16550 | Zamzam Amour |
| 41 | 11/7/19 | 16601-16650 | Wahida Omar |
| 42 | 11/7/19 | 16701-16750 | Mtumwa Bande |
| 43 | 11/7/19 | 16751-16800 | Ali Omar |
| 44 | 11/7/19 | 16851-16900 | Asha Hussein |
| 45 | 11/7/19 | 16901-16950 | Asha Said |
| 46 | 12/7/19 | 16951-17000 | Fatma Salum |
| 47 | 12/7/19 | 17001-17050 | Bimkubwa Khatib |
| 48 | 15/7/19 | 17151-17200 | Maulid /A/ Maulid |
| 49 | 15/7/19 | 17101-17150 | Zulfa Abdi |
| 50 | 15/7/19 | 17201-17250 | Masemo Ahmada |
| 51 | 16/7/19 | 17251-17300 | Mwanamanga Juma |
| 52 | 17/7/19 | 17551-17600 | Asha Said |
| 53 | 17/7/19 | 1769-17650 | Khadija Kessi |
| 54 | 19/7/19 | 17801-17850 | Wahida Omar |
| 55 | 22/7/19 | 18001-18050 | Ali Omar |
| 56 | 23/7/19 | 18151-18200 | Masemo Ahmada |
| 57 | 23/7/19 | 19201-19250 | Maulid /A/ Maulid |
| 58 | 24/7/19 | 18251-18300 | Asya Omar Makame |
| 59 | 1/8/19 | 19051-19100 | Mwanamanga Juma |
| 60 | 1/8/19 | 19101-19150 | Mwanamanga Juma |
| 61 | 14/8/19 | 19901-19950 | Miski Bakar |
| 62 | 16/8/19 | 20401-24450 | Masemo Ahmada |
| 63 | 16/8/19 | 14051-14100 | Miski Bakar |
| 64 | 16/8/19 | 18901-18950 | |
| 65 | 20/8/19 | 17701-17750 | Bimkubwa Khamis |
| 66 | 20/8/19 | 19001-19050 | Bimkubwa Khamis |
| 67 | 9/9/19 | 22601-22650 | Fatma Salum |
| 68 | 10/9/19 | 07151-07200 | Mtumwa Bande |
| 69 | 10/9/19 | 07351-07400 | Ali Omar |
| 70 | 10/9/19 | 10701-10750 | Ali Omar |
| 71 | 10/9/19 | 11151-11200 | Rahma Kwacha |
| 72 | 10/9/19 | 33351-33400 | Asha Juma |
| 73 | 10/9/19 | 33451-33500 | Seif Iddi |
| 74 | 5/9/19 | 22051-22100 | Asha Hussein |
| 75 | 16/9/19 | 23851-23900 | Mtumwa Bande |
| 76 | 9/10/19 | 00151-00200 | Omari Amani |
| 77 | 16/10/19 | 01951-02000 | Bimkubwa Khatib |
| 78 | 17/10/19 | 03051-03100 | Omari Amani |
| 79 | 6/11/19 | 04501-04550 | Asha Hussein |

## KIAMBATISHO NAMBARI 2: Vitabu vya stakabadhi ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi - Baraza la Manispaa ya Magharibi " A "

| Namba | Mtiririko wa nambari ya Stakabadhi | Aliyekabidhiwa Kitabu |
|---|---|---|
| 1 | 11801-11850 | MOHD ISMAL |
| 2 | 11851-11900 | MOHD ISMAL |
| 3 | 12901-12950 | SUBIRA JUMA ALI |
| 4 | 13401-13450 | MOHD ISMAL |
| 5 | 14401-14450 | FATMA ALI KILOKO |
| 6 | 12001-12050 | MOHD ISMAL |
| 7 | 12051-12100 | NAOMI NASSOR ALI |
| 8 | 13501-13550 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 9 | 13551-13600 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 10 | 13851-13900 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 11 | 18551-18600 | SUBIRA JUMA ALI |
| 12 | 21501-21550 | SUBIRA JUMA ALI |
| 13 | 27501-27550 | MDAMO MAKAME SIMBA |
| 14 | 27501-27550 | MDAMO MAKAME SIMBA |
| 15 | 27901-27950 | MOHD ALI MOHD |
| 16 | 30951-31000 | MOHD ALI MOHD |
| 17 | 33551-33600 | ABDUL-MALIK SEF ISSA |
| 18 | 33951-34000 | MOHD ALI MOHD |
| 19 | 35201-35250 | MOHD ALI MOHD |
| 20 | 35251-35250 | ASHA MOHD OTHMAN |
| 21 | 36101-36150 | NDAMO MAKAME SIMBA |
| 22 | 36401-36500 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 23 | 36501-36500 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 24 | 36751-36800 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 25 | 37801-37850 | ABDUL-MALIK SEF ISSA |
| 26 | 37851-37900 | ABDUL-MALIK SEF ISSA |
| 27 | 37951-38000 | ABDUL-MALIK SEF ISSA |
| 28 | 39651-39700 | IDD OTHMAN MGOMBA |
| 29 | 28651-28700 | KHATIB HAJI KHATIB |
| 30 | 28751-28800 | KHADIJA SALUM KHEIR |
| 31 | 28801-28850 | KHADIJA SALUM KHEIR |
| 32 | 28851-28900 | KHADIJA SALUM KHEIR |
| 33 | 30551-30600 | ABDUL-MALIK SEF ISSA |
| 34 | 30851-30900 | YUSSUF YAHYA MUHOJA |
| 35 | 30501-30550 | ABDULRAHMAN H. KATIB |
| 36 | 30601-30600 | ABDULRAHMAN H. KATIB |

| | | |
|---|---|---|
| 37 | 30801-30850 | ABDULRAHMAN H. KATIB |
| 38 | 3125-31300 | FAIDA MASOUD ABDALLA |
| 39 | 31301-31350 | FAIDA MASOUD ABDALLA |
| 40 | 31351-31400 | FAIDA MASOUD ABDALLA |
| 41 | 31401-31450 | FAIDA MASOUD ABDALLA |
| 42 | 31551-31600 | KHADIJA HASSAN HAMAD |
| 43 | 30501-30550 | ABDULRAHMAN H. KATIB |

**KIAMBATISHO NAMBARI 3: Vitabu vya stakabadhi ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi Baraza la Manispaa ya Magharibi " B "**

| Nambari | Tarehe | Mtiririko wa nambari za stakabadhi |
|---|---|---|
| 1 | 19/9/2019 | 72101-72200 |
| 2 | 18/9/2019 | 72601-72700 |
| 3 | 18/902019 | 72701-72800 |
| 4 | 20/9/2019 | 72601-7300 |
| 5 | 25/9/2019 | 7401-74300 |
| 6 | 26/9/2019 | 74501-74600 |
| 7 | 27/9/2019 | 74801-74900 |
| 8 | 2/10/2019 | 76101-76200 |
| 9 | 17/7/2019 | 52001-52100 |
| 10 | 17/7/2019 | 72101-52200 |
| 11 | 18/7/2019 | 52501-52600 |
| 12 | 9/7/2019 | 43901-44000 |
| 13 | 11/7/2019 | 49201-49300 |
| 14 | 11/7/2019 | 49301-49400 |
| 15 | 30/7/2019 | 55201-55300 |
| 16 | 9/8/2019 | 59801-59900 |
| 17 | 19/8/2019 | 63001-63100 |
| 18 | 22/8/2019 | 63401-63500 |
| 19 | 22/8/2019 | 63501-53600 |
| 20 | 2/9/2019 | 68201-68300 |
| 21 | 3/9/2019 | 68701-68800 |
| 22 | 10/9/2019 | 70201-70300 |
| 23 | 10/9/2019 | 70301-70400 |
| 24 | 10/9/2019 | 70601-70700 |
| 25 | 17/10/2019 | 79801-79900 |
| 26 | 18/10/2109 | 80101-80200 |
| 27 | 18/10/2019 | 80201-80300 |
| 28 | 11/11/2019 | 86501-86600 |
| 29 | 11/11/2019 | 86601-86700 |
| 30 | 12/11/2019 | 87601-87700 |
| 31 | 18/11/2019 | 88601-88700 |
| 32 | 18/11/2019 | 88801-88900 |
| 33 | 19/11/2019 | 88901-89000 |
| 34 | 21/11/2019 | 89701-89800 |
| 35 | 21/11/2019 | 89801-89900 |
| 36 | 20/1/2020 | 94501-94600 |

| | | |
|---|---|---|
| 37 | 24/1/2020 | 95001-95100 |
| 38 | 24/1/2020 | 95301-95400 |
| 39 | 3/3/2020 | 4701-4800 |
| 40 | 9/4/2020 | 12401-12500 |
| 41 | 21/4/2020 | 14501-14600 |
| 42 | 24/4/2020 | 15501-15600 |
| 43 | 28/4/2020 | 16901-17000 |
| 44 | 8/5/2020 | 24801-24900 |
| 45 | 13/5/2020 | 26301-26400 |
| 46 | 13/5/2020 | 26401-26500 |
| 47 | 14/5/2020 | 27001-27100 |
| 48 | 26/5/2020 | 32001-32100 |
| 49 | 8/6/2020 | 34901-35000 |
| 50 | 12/6/2020 | 35401-35500 |
| 51 | 15/6/2020 | 36601-36700 |
| 52 | 18/6/2020 | 37101-37200 |
| 53 | 19/6/2020 | 37400-37500 |
| 54 | 25/6/2020 | 38401-38500 |
| 55 | 30/6/2020 | 39701-39800 |
| 56 | 30/6/2020 | 39801-39900 |
| 57 | 30/6/2020 | 40101-40200 |
| | | |

**KIAMBATISHO NAMBARI 4: Watumishi ambao mikataba yao imemaliza muda Baraza la Manispaa ya Magharibi " B "**

| NAM. | JINA LA MFANYAKAZI | DHAMANA | KIWANGO CHA MSHAHARA (SHS) | TAREHE YA KUANZA MKATABA | TAREHE YA KUMALIZA MKATABA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Sabra Maulid Mtoro | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 2 | Maryam Bakari Mussa | M/Sheria | 200,000 | 8/1/2018 | 8/1/2019 |
| 3 | Radhiya Nassir Alawi | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 4 | Zainab Khamis Mbarouk | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 5 | Rehema Othman Ali | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 6 | Fatma Muhidin Nanyup | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 7 | Shani Khamis Uledi | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 8 | Amina Ramdhan Iddi | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 9 | Fatma Abdallah Hassan | Tehama | 350,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 10 | Fatma Bakari Makame | Msafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 11 | Asha Salum Matunda | Msafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 12 | Fatma Abdallah Ali | Msafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 13 | Amina Nuhu Ali | Karani Mapato | 400,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 14 | Maryam Khamis Nassor | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 15 | Asha Salum Mohd | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 16 | Chausiku Abdalla Sama | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 17 | Maryam Suleiman Haji | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 18 | Kiwaliki Vuai Hassan | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 19 | Najma Issa Fatawi | Karani Mapato | 180,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 20 | Aziza Abdalla Hassan | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 21 | Jina Hamdu Shaka | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 22 | Ana Selevesta Andrea | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 23 | Mwanakhamis Idd Khamis | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 24 | Fatma Ali Jecha | Karani Mapato | 180,000 | 1/1/2018 | 30/6/2019 |
| 25 | Somea Rashid Ali | Usafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 26 | Fatma Tongoa Issa | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 27 | Ali Othman Ali | Fundi Magari | 11,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 28 | Jaha Faki Khalfani | Usafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 29 | Hafsa Muhammed Makame | Tehama | 300,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 30 | Ali Mwinyi Mwalim | Fundi Magari | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 31 | Othman Shaaban Mabara | Mkaguzi | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |
| 32 | Abdul-Majid Ali Salum | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 |